# MWONGOZO WA UFUGAJI BORA WA KUKU WA ASILI



TOA ZAWADI PIA

HEIFER®
INTERNATIONAL
TANZANIA

**Mwongozo huu wa ufugaji kuku wa Asilia umezinduliwa rasmi leo tarehe 1 Agosti 2009 wakati wa sikukuu ya Wakulima Tanzania mjini Mbeya**

TOA ZAWADI PIA

HEIFER®

INTERNATIONAL

TANZANIA

# MWONGOZO WA UFUGAJI KUKU WA ASILI KWA WAKULIMA WA TANZANIA

***Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kutoa maelekezo rahisi juu ya ufugaji bora wa kuku wa Asili na jinsi kuku hao wanavyoweza kumsaidia mkulima mfugaji kuondokana na umasikini.***

TOA ZAWADI PIA

HEIFER® INTERNATIONAL

**TANZANIA**

Chapisho la pili katika lugha ya Kiswahili 2010

**© 2010 Heifer International Tanzania**

# Yaliyomo


Shukrani i
Dibaji ii
Utangulizi iii
*Utume wa Heifer International* *iv*
*Dira ya Heifer International* *iv*
*Falsafa ya Heifer International* *iv*
*Nguzo za Heifer International* *vi*

**Mada ya 1: Sifa, Faida na Changamoto za ufugaji wa kuku wa Asili** **1**
*Sifa za kuku wa Asili* *1*
*Faida za ufugaji wa kuku wa Asili* *2*
*Mapungufu ya kuku wa Asili* *2*
*Changamoto katika ufugaji kuku wa Asili* *3*

**Mada ya 2: Kabila za kuku wa Asili** **4**
*Kuchi* *4*
*Umbo la kati* *4*
*Ching'weke* *4*
*Singamagazi* *4*
*Mbeya* *5*
*Pemba* *5*
*Unguja* *5*
*Aina nyingine* *5*

**Mada ya 3: Mifumo ya ufugaji kuku wa Asili** **7**
*Ufugaji huria* *7*
*Ufugaji nusu huria* *8*
*Ufugaji wa ndani* *9*

**Mada ya 4: Maandalizi ya ufugaji kuku wa Asili** **11**
*Banda bora* *11*
*Sifa za banda bora la kuku* *12*
*Kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi* *12*
*Njia zitumikazo katika kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi* *13*
*Wakati muafaka wa kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi* *13*
*Faida ya kuondoa kuku wasiofaa kwenye kundi* *13*
*Umri wa kupevuka* *14*
*Uwiano wa mitetea na majogoo* *14*
*Fuga kuku upate faida* *14*

**Mada 5: Vifaa muhimu ndani ya banda la kuku** **15**
*Vyombo vya chakula* *15*
*Vyombo vya maji* *16*
*Viota* *16*
*Vichanja vya kupumzikia na kulala* *17*
*Uwekaji wa matandiko* *17*

**Mada ya 6: Vyakula na ulishaji wa kuku wa Asili 19**

*Baadhi ya vyakula vyenye asili ifuatazo pia vinafaa kulisha kuku* 20

**Mafunzo kwa vitendo:** 21
- **Washiriki wachanganye chakula cha kuku kwa kufuata vipimo walivyoelekezwa kwenye nadharia.**

**Mada ya 7: Utagaji, Uatamiaji na Uanguaji wa vifaranga 22**

*Fuata utaratibu ufuatao kuhifadhi mayai* 22
*Sifa za mayai ya kuatamiwa* 22
*Njia za uatamiaji na uanguaji* 23
*Uanguaji wa kubuni* 23
*Uanguaji wa asili* 24
*Kuchagua mtetea anayeweza kuatamia mayai yasiyokuwa yake* 24
*Kuwatayarisha kuku wa kuatamia* 25
*Kuwafanya kuku wengi kutotoa kwa wakati mmoja* 25
*Mbinu za kuzalisha kuku wengi kwa muda mfupi* 26
*Jinsi ya kutambua mayai yaliyo na mbegu na yasiyo na mbegu* 28

**Mafunzo kwa vitendo:** 28
- **Kutenganisha kuku(vijogoo na temba).**
- **Usafishaji wa mayai yaliyochafuka.**
- **Jinsi ya kutambua kuku wtagao na wasiotaga.**

**Mada ya 8: Uleaji wa vifaranga 29**

*Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili* 29
*Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni* 29
*Njia ya uleaji wa vifaranga kwa kutumia nishati* 30
*Njia ya uleaji wavifaranga isiyotumia nishati* 33

**Mafunzo kwa vitendo:** 38
- **Ushikaji wa kuku unaofaa.**
- **Uandaaji wa sehemu ya kulelea vifaranga.**

**Mada ya 9: Tabia mbaya miongoni mwa kuku wa Asili 39**

**Mafunzo kwa vitendo:** 39
- **Kutambua tabia zisizofaa kwenye kuku na ukataji wa midomo ya kuku.**

**Mada ya 10: Magonjwa na wadudu washambuliao kuku wa Asili 40**

*Magonjwa yashambuliayo kuku wa Asili* 40
*Kideri/Mdondo (New Castle Disease)* 40
*Ndui ya kuku (Fowl Pox)* 42
*Homa ya matumbo (Fowl Typhoid)* 43
*Mafua ya kuku (Infectious Coryza)* 44
*Kuhara damu (Coccidiosis)* 45
*Kipindupindu cha kuku (Fowl Cholera)*
*Ukosefu wa vitamini ‘A’* 46
*Wadudu washambuliao kuku wa Asili* 47
*Wadudu washambuliao ndani ya mwili* 47
*Vidusia wa nje washambuliao kuku* 48

*Athari za wadudu washambuliao kuku* 48

**Mafunzo kwa vitendo:** 49
- **Uchanjaji wa kuku ili kuzuia maradhi.**
- **Kutoa dawa ya utitiri, viroboto na chawa.**
- **Kutoa dawa za minyoo.**
- **Kusafisha mabanda ya kuku kwa kutumia dawa.**

**Mada ya 11: Tiba za asili** **50**
*Sehemu za mimea* 50
*Umuhimu wa kutumia tiba zenye asili ya mimea* 50
*Baadhi ya mimea inayotibu maradhi ya kuku* 50

**Mada ya 12: Kuweka kumbukumbu za ufugaji wa kuku wa asili** **53**
*Faida za kumbukumbu* 53
*Kumbukumbu zimegawanyika katika sehemu hizi* 53

**Mafunzo kwa vitendo:** 55
- **Uwekaji wa kumbukumbu.**

**Mada ya 13: Ujasiriamali** **56**
*Maana ya ujasiriamali* 56
*Kanuni za mfanyabiashara mtafutaji/mjasiriamali* 57
*Aina za umiliki wa biashara* 57
*Wazo la biashara* 57
*Matatizo yanayoathiri wazo la biashara* 59
*Jinsi ya kuanzisha biashara* 59
*Faida ya mchanganuo wa biashara* 60
*Vyanzo vya taarifa za biashara* 60
*Masoko* 61
*Mipango ya uwekezaji* 63

# Shukrani

Katika kukamilisha mwongozo huu, michango mbalimbali ya wadau katika sekta ya ufugaji imechangia hadi kuchapishwa kwa mwongozo huu. Hivyo tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote ambao kwa njia moja au niyingine wamechangia muda, utaalamu na hata mawazo katika mchakato mzima wa kukamilisha kitabu hiki. Kipekee kabisa tungependa kuwashukuru wafuatao:

Ndugu Bahati Nzunda, Meneja wa Programu ya Heifer Tanzania kanda ya Kusini Mashariki aliyeanzisha wazo la awali la kuwa na mwongozo wa ufugaji wa kuku asilia. Alichukua jukumu kubwa la kuanza uandishi wa awali na leo hii tunayaona matunda ya juhudi zake.

Wa pili ni Ndugu Abdul Mtumwa, Afisa wa Miradi - Heifer Tanzania kanda ya Kusini Mashariki; Ndugu Shwaib Mmbaga Afisa Mifugo Msaidizi katika wilaya ya Mkuranga na Msimamizi wa Miradi ya Heifer na Ndugu Mohamed Mfaume Afisa Mifugo Msaidizi Mkuu katika Wilaya ya Kinondoni ambao walibeba jukumu kubwa la kuhakikisha mambo muhimu ya kitaalamu yanaingizwa katika mwongozo huu.

Shukrani za dhati ziende kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, hususan Ndugu John Kaijage Mtafiti Mkuu wa Mifugo aliyekuwa na kazi ya kuhariri mwongozo huu na kuhahakikisha mambo muhimu juu ya ufugaji kuku asilia yamezingatiwa na kukubali kwake kutumia picha na matokeo ya tafiti mabalimbali alizofanya.

Shukrani pia ziende Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, waliokubali matumizi ya baadhi ya picha zao zilizomo kwenye mwongozo huu, wafanyakazi wote wa Heifer Tanzania katika kanda zote na makao makuu ya Heifer Tanzania na wakulima wafugaji kwa kukubali kupitia mwongozo huu na kutoa maoni yao.

Tunawaomba nyote mpokee waraka huu kama shukrani zetu za dhati kwenu, asanteni sana.

# Dibaji

Ufugaji wa kuku wa Asili ni jambo lisilo geni katika kaya zetu hapa nchini, lakini ufugaji uliopo sasa haujapewa umuhimu kuweza kuzinufaisha familia na hata kuchangia katika pato la taifa kwa kiasi kikubwa. Kuku wa Asili wamekuwa wanafugwa kama mazoea tu na kwa matumizi madogo madogo kama ya kitoweo na kujikimu kwa tatizo liliopo kwa wakati huo.

Mwongozo huu umeandaliwa kuweza kubadili mtazamo huo na kuweza kutoa maelekezo rahisi kwa wafugaji jinsi gani kuku wa Asili anaweza kumsaidia mkulima kuondokana na umasikini. Inakadiriwa kuwa wapo kuku asilia wapatao milioni 56 hapa nchini ambao wanachangia asilimia 30 ya pato la jumla (GDP) litokanalo na mifugo (5.9%). Huu ni ushahidi tosha kuwa iwapo kuku wa Asili watafugwa na kuhudumiwa kwa misingi imara basi inawezekana kuongeza pato hilo maradufu na kuleta tija kwa familia nyingi.

Changamoto kubwa inayowakabili wafugaji wa kuku wa Asili ni magonjwa ya kuambukiza na vifo vingi vya vifaranga. Kuku wengi hufa wakati wa magonjwa ya mlipuko hususan Mdondo, kutokuwepo nyumba maalum ya kuku kwa ajili ya kutaga na kulelea vifaranga na kutopata elimu ya ufugaji wa kuku wa asili kibiashara. Mwongozo huu unalenga kuleta mapinduzi ya hali hiyo kwa kujaribu kuelekeza hatua zipi zifuatwe ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo kubwa na kuleta tija kwa familia. Tumeweza kuona katika miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Heifer ni kwa kiasi gani ufugaji wa kuku wa Asili umeweza kusaidia familia nyingi kuondokana na umasikini. Hivyo tunao uhakika kuwa mwongozo huu utaweza kuwasaidia hata wale wasiokuwa katika miradi yenye ufadhili kwa kuweza kujisomea na kufuata taratibu zote hata kuweza kupata faida kutokana na ufugaji wa kuku wa Asili.

Mwongozo huu tofauti na iliyotangulia, umeandaliwa katika mazingira rahisi na unamwezesha mtu yeyote kujisomea na kutekeleza yaliyomo. Mwongozo huu umeandaliwa kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali wenye njozi ya kuona kuku wa Asili anachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa na kuondoa umasikini katika ngazi ya kaya.

Mwongozo huu una mada zinazoelekeza ufugaji ulio bora wa kuku wa Asili ikiwemo jinsi ya kutambua ubora wa kuku wanaostahili kufugwa, mifumo mbalimbali itakayoweza kutumika na mapungufu yaliyomo katika ufugaji na jinsi ya kuyatatua. Vilevile mwongozo huu unaelezea juu ya utagaji na utunzaji wa mayai, uatamiaji na uanguaji wa vifaranga na njia za kulea vifaranga ili kuzuia vifo katika hatua za awali. Pia mwongozo unaelezea lishe kwa kuku wa Asili, mbinu za kuzalisha kuku wengi kwa muda mfupi ili kuweza kupata faida katika ufugaji, magonjwa muhimu ya kuku wa asili na jinsi ya kuyakinga na uwekaji wa kumbukumbu za ufugaji.

Ni imani yangu kuwa mwongozo huu utaleta mabadiliko makubwa katika eneo hili la ufugaji kuku wa asili na kuziwezesha familia zetu kumfuga kuku huyu kwa faida na si kuishi naye na hatimaye kuchangia katika kuongeza pato la mfugaji na kuwa na uhakika wa chakula kwa familia.



**Peter K. Mwakabwale**
**Mkurugenzi**
**Heifer International Tanzania**

## Shirika la Mitamba Tanzania (Heifer International Tanzania)

Heifer International (Shirika la Kimataifa la Mitamba) ni taasisi isiyo ya kiserikali ya huduma za kibinadamu iliyojitoa kumaliza njaa na umasikini duniani na kutunza ardhi kwa kugawa mifugo, miti, mafunzo na rasilimali nyingine kusaidia familia masikini ulimwenguni kuweza kujitegemea na kuinua kiwango chao cha maisha. Heifer International ilianzishwa mwaka 1944 huko nchini Marekani mara baada ya vita kuu ya pili ya dunia. Mwasisi wake alikuwa mwinjilisiti Dan West. Leo hii, kazi zake zimefanyika katika nchi 125 duniani na majimbo 38 ya Marekani.

Mwaka 1974, Heifer International iliamua kuingia Afrika na Tanzania ikawa ndiyo nchi ya kwanza kuanzisha miradi na kazi za Heifer katika bara la Afrika. Uamuzi wa kuingia Tanzania ulifuatia mualiko uliofanywa na Serikali ya Tanzania kwa lengo la kuboresha maisha ya wakulima walioko vijijini kwa kugawa mitamba katika vijiji vya Ujamaa wakati vinaanzishwa. Lakini baadae, Heifer iliona kuwa uwezekano wa kulifikia lengo utakuwepo iwapo tu italengwa familia moja moja, badala ya jamii kwa ujumla.

Mwaka 1981, Heifer International – Marekani ilishauriana na serikali kuanzisha utaratibu mpya wa kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ambao ndio walio wengi kwa kutumia mfumo na falsafa ya Heifer ya dhamana ya ***'Kopa ng'ombe lipa ng'ombe',*** ikilenga kuboresha maisha ya familia moja moja zenye kipato cha chini.

Kuanzia hapo, Heifer International Tanzania, imekuwa inatekeleza miradi kwa kutumia mikakati thabiti ambayo, si tu inayolenga katika utoaji wa mitamba, bali kukuza na kutoa aina mbali mbali za wanyama ikiwemo, ng'ombe na mbuzi wa maziwa, mbuzi wa nyama, nguruwe, kuku wa asili, punda na ngamia. Miradi mingine ni ya ufugaji nyuki, ufugaji wa samaki na utunzanji wa mazingira. Heifer pia huchangia juhudi za ulimwengu katika masuala mtambuke ya jinsia na kupunguza kasi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na kutoa huduma kwa wale wanaoishi na VVU na UKIMWI, mayatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Kazi zote za Heifer zinafanyika kwa ushirikiano mkubwa kati yake na serikali, taasisi za kidini na taasisi za kijamii katika juhudi za kusaidia familia duni kwa kuwapatia mifugo, mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kupunguza makali ya umasikini na njaa.

**Utume wa Heifer:**

Kushirikiana na jamii kutokomeza njaa na umasikini pamoja na kuitunza ardhi

**Dira ya Heifer:**

Jamii ya ulimwengu inayoishi pamoja kwa amani na uwiano mzuri wa mgawanyo wa rasilimali za sayari yenye utajiri mkubwa.

**Falsafa ya Heifer:**

'Toa Zawadi kwa Wengine' ni mkakati na mhimili mkuu wa falsafa ya Heifer katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo endelevu – kadiri watu wanavyogawana uzao wa mifugo yao, ikiambatana na kubadilishana maarifa, rasilimal na stadi zao, kunajengeka mtandao imara wenye matumaini, heshima na moyo wa kujitegemea unaosambaa ulimwenguni kote

**Maeneo ya Kipaumbele:**

1. Uimarishaji wa taasisi ya Heifer Tanzania
2. Usawa wa Jinsia na elimu ya VVU na UKIMWI
3. Mandeleo ya kibiashara ya kijamii
4. Kukuza ushirikiano na wadau wengine pia mitandao mbalimbali
5. Kukuza utunzaji wa mazingira
6. Kuboresha hali za maisha ya wahitaji wenye kipato cha chini

**Tunafanyaje kazi:**

Katika juhudi za kutimiza adhima zake, Heifer International Tanzania inafanya kazi zake kwa ushirikiano mkubwa na serikali ya Tanzania kupitia wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Halmashauri za wilaya na wadau wengine. Heifer inatoa wanyama na mafunzo na Halmashauri zinachangia wafanyakazi wa ugani wa mifugo wanaosimamia miradi na wadau wengine wanajitoa kudhamini na kuratibu utekelezaji wa miradi kwa kushirikiana na kamati za miradi.

Familia duni zimekuwa zinawezeshwa kwa kupewa wanyama mbalimbali. Hadi leo Heifer International Tanzania inajihusisha na utoaji wa wanyama wafuatao:

- Ng'ombe wa maziwa
- Mbuzi wa maziwa
- Mbuzi wa nyama
- Nguruwe
- Kuku wa asili

- Punda
- Ngamia
- Nyuki
- Samaki

Vilevile shirika linasisitiza shughuli za ufugaji ziende sambamba na shguhuli za Kilimo Hai na uhifadhi wa mazingira.

Heifer International Tanzania imetekeleza miradi katika mikoa yote 21 ya Tanzania bara na 5 Tanzania visiwani. Kati ya wilaya 127 nchini, Heifer imetekeleza miradi katika wilaya 106.

**Nini kinafanya Heifer kuwa ya kipekee?**

***'Toa Zawadi kwa Wengine,*** ni mfano wa kipekee ambapo familia moja inayopata mfugo na ujuzi, inakubali kutoa uzao wa kwanza wa mfugo ambao ni jike kwenda kwa familia nyingine hitaji. Mlolongo huu huendelezwa na kuwasaidia maelfu ya familia wahitaji na kuwapunguzia makali ya maisha.

Lakini pia, ubora wake wa hali ya juu ni ule utokanao na urahisi na ufanisi wake. Kwa kifupi ni ule utekelezaji wa kimkakati endelevu wa ***'Familia moja kwa wakati mmoja'.*** Hali hii imepelekea taasisi nyingi kuiga na kuanza kutumia mfumo huu. Hali hii imeweza kutoa changamoto kubwa kwa taasisi mbalimbali zinazolenga kuwezesha jamii kujitegemea.

Mkakati wenye matokeo mazuri unaowezesha kupunguza utegemezi katika miradi ya Heifer, hususani, wataalamu wa ugani na wafadhili, ni ule wa kujengea uwezo wakulima rika na wahudumu wa afya za wanyama vijijini. Watu hawa ambao ni wa kujitolea, wapo katika kila eneo la mradi na wanasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa ya mifugo yanayoweza kuzuilika.

Matokeo ya miradi inayofadhiliwa na Heifer yanaonekana wazi nchini. Miradi imewezesha familia nyingi kuboresha afya na kipato chao. Kutokana na kipato, familia nyingi zimeweza kuboresha nyumba zao na hata kujenga za kisasa, kulipia watoto wao ada za shule, kulipia huduma za afya na hata mahitaji mengine muhimu ya kifamilia. Pia, miradi hii imewezesha kutoa ajira vijijini na kupunguza uhamiaji mijini, imeboresha mazingira na uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara.

Heifer itaendelea kutumia mkabala wa jumla wa maendeleo kuwawezesha wanajamii waliopo vijijini katika kuboresha maisha yao binafsi. Familia walengwa, wanawezeshwa kutambua mahitaji na changamoto zao, kuamua miradi inayowafaa, kupanga na kutekeleza miradi itakayoboresha maisha yao.

**Nguzo za Heifer International:**

Iwapo utawauliza wadau wa Heifer, 'ni nini kanuni za msingi ambazo kwazo zinajenga maisha yao?' wengi watasema 'nguzo za Heifer.' Nguzo hizi zinasisimua hekima za makundi na mtazamo binafsi na kutia moyo, changamoto na matendo yenye mwelekeo na matokeo.

Nguzo hizi zinafafanua maneno '***TOA ZAWADI PIA'*** ambayo yanatoa mwanga unaofanya Heifer kuwa ya mfano wa pekee na miradi yake kuwa ya endelevu. Nguzo hizo ni:



**Toa Zawadi kwa Wengine:**

Huu ni msingi wa kuonyesha kwa vitendo falsafa ya Heifer ya kupendana, kushirikiana na kutunzana. Kila familia inayopokea zawadi kutoka Heifer nayo hukubali kutoa zawadi ya uzao jike wa kwanza kwa familia nyingine hitaji ikiwa ni pamoja na elimu na ujuzi waliopata kutokana na mafunzo waliyohudhuria.




**Onyesha Uwajibikaji:**

Walengwa huamua matakwa yao wenyewe, hupanga mipango ya miradi, huchambua walengwa, hutekeleza miradi kama inavyotakiwa, hufuatilia maendeleo yake, hutunza kumbukumbu, hutoa taarifa za maendeleo yake na kutathmini mradi kwa kushirikiana na wadau wote.



**Angalia Kushirikishana na Kutunzana:**

Heifer inaamini kuwa matatizo ya dunia yanaweza kutatuliwa endapo tu watu wote watawajibika kwa kushirikiana kwa kila walichonacho na kujali wengine wenye dhiki. Kushirikiana na kutunzana pia kunaonyesha wajibu wetu kwa matunzo ya wanyama katika miradi ya Heifer na haja ya kutenda haki kwa watu wote.



**Zingatia Mipango Endelevu na Kujitegemea:**

Miradi inayofadhiliwa na Heifer huwa na kipindi maalumu cha utekelezaji. Wanakikundi husaidiwa kuweka malengo ya kujiandaa kujitegemea wenyewe kwa kutumia michango ya wanachama, kujishughulisha na kazi za uzalishaji, kutafuta wafadhili wengine na kushirikiana na miradi mingine. Heifer inatambua kuwa mara nyingi kujitegemea kwa vikundi huwa rahisi endapo vikundi vyenyewe vitaanzisha na kubuni miradi tofauti itakayoweza kuwaongezea kipato.



**Angalia Masuala ya Jinsia na Familia:**

Heifer inatilia mkazo suala la ushirikiano na mahusiano katika familia na pia kufanya maamuzi juu ya umiliki na usimamizi wa mifugo, nguvukazi na kufaidi matunda ya mradi kwa pamoja huku mila na desturi za wahusika zikizingatiwa. Kipaumbele kwenye ufadhili wa miradi hutolewa kwa miradi inayolenga familia moja moja na kuhakikisha kuwa familia nzima inahusika katika utekelezaji wake.



**Wekeza Kwenye Lishe na Kipato:**

Mifugo huchangia moja kwa moja kuboresha lishe na ustawi wa familia kwa kuinua kipato na kutoa lishe. Bidhaa zitokanazo na mifugo hutumiwa na familia na ziada huuzwa na kutoa dhamana ya muda mrefu kiuchumi, elimu, makazi na tiba na wakati huo huo kutumika kama akaunti ya akiba kwa nyakati za dharura.



**Andaa Usimamizi Bora wa Mifugo:**

Afya bora ya mifugo ni muhimu ili kuweza kufikia malengo kwa ufanisi. Heifer husisitiza ubora wa mabanda, malisho bora, maji ya kutosha na uzalishaji wenye tija ili mifugo iwe na afya na uzalishaji mzuri. Pia mifugo inayotolewa iendane na hali halisi ya eneo inapopelekwa.



**Daima Zingatia Wahitaji Halisi na Haki:**

Heifer ni mshirika kwa watu ambao huhitaji kweli fursa ya kuwa na maisha bora. Wanakikundi huandaa vigezo muhimu vya kuwawezesha kupata familia hitaji zaidi ili ziweze kushiriki katika mradi. Wahitaji halisi wanaolengwa na kupewa kipaumbele ni wale wenye vipato vya chini na rasilimali duni. Hawa ni pamoja na wajane, wazee, vilema, yatima na watoto walio katika mazingira magumu. Ufadhili hutolewa pasipo kujali imani ya mtu, rangi, itikadi za kisiasa wala kabila.



**Itikia Wito wa Kuboresha Mazingira:**

Wanyama na mimea hutegemeana kwa samadi, nyasi na masalia ya mazao kwa mzunguko na kuhakikisha kuwa mifugo haichangii ongezeko la kuharibika kwa ardhi yetu bali inachangia utunzaji wake na kuiboresha.


Heifer hutoa mifugo kama njia mojawapo ya kuboresha mazingira kwa kushawishi wafugaji kufugia ndani na pia kuwa na mifugo michache iliyo bora. Haya hufanyika katika juhudi za kuzuia mmomonyoko wa ardhi, kusisitiza

matumizi ya samadi ili kurutubisha udongo, kufanya usafi, kutunza misitu na kupanda miti ili kupata kuni, mbao, kivuli na kutunza wanyama pori pamoja na vyanzo vya maji.



**Pamoja tushiriki kikamilifu katika maamuzi:**

Heifer hufanya kazi na vikundi katika ngazi za vijiji. Vikundi hivi huhamasishwa kufanya kazi kwa pamoja chini ya uongozi waliouweka wenyewe na kupanga mipango yao wenyewe iliyo mizuri na inayotekelezeka na ambayo inawahusisha walengwa wote katika kufanya maamuzi. Ushirikishwaji huwezesha walengwa kumiliki mradi na vikundi kuwa na madaraka ya maamuzi yote muhimu kwenye mradi.



**Imarisha Mafunzo na Elimu ili kuongeza ufanisi:**

Vikundi hujengewa uwezo wa kutoa maamuzi juu ya aina ya mafunzo wanayohitaji. Mafunzo mengi huhusisha masomo rasmi kama ya darasani au yasiyo rasmi kama ya wafugaji kutembeleana na kubadilishana uzoefu na ujuzi na kushiriki katika maonesho mbalimbali. Mafunzo hutolewa kwa vitendo zaidi kwa washiriki kutumia mikono yao kuliko nadharia ya madarasani.



**Andaa wahusika Kiroho:**

Mambo ya kiroho hufanywa kwa pamoja na watu wote bila kujali dini na imani zao. Mambo ya kiroho hudhihirishwa na tunu za jamii husika, imani ya pamoja inayohusu tunu na maana yake katika maisha, hali ya kuwaunganisha na dunia na maono ya baadaye. Hii husaidia kuleta maelewano mazuri na uunganishi wa kikundi na kuleta imani, mategemeo mema na hali ya kuwajibika kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya maisha mazuri ya baadaye.

# Mada ya 1: Sifa, Faida na Changamoto za Ufugaji wa Kuku wa Asili

Kuku wa Asili ni wale ambao wamekuwepo hapa nchini kwa miaka mingi na damu yao haijachanganyika na ya kuku wa kigeni. Kuku hawa wana rangi na maumbo mbali mbali. Idadi ya kuku wa Asili hapa Tanzania inakadiriwa kufikia milioni 56. Kati ya kaya milioni 3.8 zinazojishughulisha na kilimo nchini, kaya milioni 2.3 hujishughulisha na ufugaji wa kuku wa asili. Kwa kawaida ufugaji wa kuku wa Asili hapa nchini kwetu Tanzania hufanywa na wafugaji wadogo wadogo wanaoishi kando kando ya miji na wale wanaoishi vijijini. Kuku hawa hufugwa huria *(free-range),* yaani hufungiwa ndani nyakati za usiku na hufunguliwa asubuhi ili wajitafutie chakula.

Kuku hawa hutoa mazao machache sana yaani nyama na mayai, kwa mfano kuku mmoja hutaga kiasi cha mayai 40-60 kwa mwaka badala ya 100-150 iwapo atatunzwa vizuri. Pia uzito wa kuku hai ni wa chini sana, wastani wa kilo 1.0–1.5 katika umri wa zaidi ya miezi 6 badala ya kilo 1.8–2.5 iwapo atatunzwa vizuri.

**Sifa za Kuku wa Asili:**

a. Wastahimilivu wa magonjwa, lakini ni muhimu wakikingwa na baadhi ya magonjwa ya kuku kama mdondo, ndui ya kuku nk. ili kuweza kuwaendeleza.

b. Wana uwezo wa kujitafutia chakula ardhini, lakini ili kuwaendeleza ni lazima kuwapa chakula bora cha ziada.

c. Wana uwezo wa kuatamia mayai, kutotoa, kulea vifaranga na ustahimilivu wa mazingira magumu (ukame, baridi nk).

d. Nyama na mayai yake vina ladha nzuri kuliko kuku wa kisasa.

e. Kwa kiasi fulani wana uwezo wa kujilinda na maadui kama vile mwewe.

Pamoja na sifa hizi ni muhimu kuku hao wakapewa matunzo mazuri, wawekwe kwenye mabanda mazuri na imara, pia wapewe maji na chakula cha kutosha.



*Kuku wa Asili wakila chakula.*

**Faida za Ufugaji wa Kuku wa Asili:**

a. Chakula – nyama ya kuku na mayai hutumika kama chakula muhimu cha wanadamu, chenye protini.
b. Chanzo cha kipato – mkulima hupata fedha akiuza kuku au mayai.
c. Chanzo cha ajira – ufugaji wa kuku hutoa ajira kwa jamii.
d. Kuku hutumika kwenye shughuli za ndoa kama vile kutoa mahari na pia ni kitoweo muhimu katika sherehe hizo.
e. Gharama nafuu za kuanzisha na kuendesha mradi huu.
f. Ni kitoweo rahisi na chepesi kwa wageni kuliko wanyama wakubwa kama ng'ombe au mbuzi.
g. Ni kitoweo kisichohitaji hifadhi, hutumika mlo mmoja au miwili na kumalizika.
h. Kuku na mayai hutumika kwa tiba za asili.
i. Jogoo hutumika kama saa anapowika nyakati za alfajiri na majira mengine ya siku.
j. Hutuhabarisha iwapo kiumbe kigeni au cha hatari kwa mlio maalum wa kuashiria hatari.
k. Mbolea – kinyesi cha kuku kinaweza kutumika katika kurutubisha mashamba ya mazao na mabwawa ya samaki.
l. Kuendeleza kizazi cha kuku wa asili hapa nchini.
m. Soko lipo la uhakika, ukilinganisha na kuku wa kisasa kwani nyama na mayai yake hupendwa zaidi na walaji.
n. Manyoya ya kuku hutumika kama mapambo, pia huweza kutumiaka kutengenezea mito ya kulalia na kukalia.
o. Shughuli za utafiti – kuku wanatumika katika tafiti nyingi za baiolojia, kama kutambua mambo ya lishe.
p. Shughuli za viwandani:
    - Mayai yenye mbegu ya jogoo hutumika katika kutengeneza dawa za chanjo.
    - Magamba ya mayai yanaweza kutumika katika utengenezaji wa vyakula vya wanyama.
    - Kiini cha njano cha mayai kinaweza kutumika kutengeneza mafuta ya kuoshea nywele *(shampoo).*

**Mapungufu ya Kuku wa Asili:**

a. Hutaga mayai madogo wastani wa gramu 47 ambapo kuku wa kisasa wastani wa gramu 55, aidha hutaga mayai machache wastani wa mayai 60 kwa mwaka ambapo kuku wa kisasa huweza kutaga hadi  mayai 300 kwa mwaka.
b. Ukuaji taratibu – kuku wa asili hukua taratibu kutokana na lishe duni. Kutokana na hali hiyo kuku huchukua muda mrefu (miezi sita) kufikia uzito wa kuchinjwa (kilo 1 - 1.5). Hali hii pia hufanya faida ya ufugaji wa kuku wa asili kuchukua muda mrefu kupatikana.
c. Nyama yake ni ngumu (huchukua muda mrefu kuiva) ikilinganishwa na kuku wa kisasa.

**Changamoto katika ufugaji kuku wa asili:**

a. Mabanda: Ukosefu wa mabanda bora.

b. Wezi, wanyama na ndege hushambulia kuku.

c. Magonjwa: kama mdondo na ndui huathiri ufugaji wa kuku.

d. Tabia na miiko ya baadhi ya jamii. Baadhi ya jamii za makabila hapa nchini huona ufugaji wa kuku kama ni kitu duni.

e. Upatikanaji haba wa chanjo za magonjwa kama vile, mdondo, ndui, homa ya matumbo.

## Mada ya 2: Kabila za Kuku wa Asili

Si rahisi kuweza kupata kabila halisi *(Pure breed)* au kizazi halisi *(Pure line)* za kuku wa Asili kutokana na mazingira ya muingiliano wa vizazi kati ya aina mbalimbali za kuku hao. Hata hivyo kuku hawa wana tofauti za kimaumbile zilizosababisha kuwepo kwa kabila mbalimbali baina yao. Kabila hizi pia zinahusishwa kwa kiasi kikubwa na eneo kuku hao wanakotoka.

Kutokana na muingiliano wa vizazi, maumbile hayo yanaweza yakajitokeza kwenye aina mbalimbali za kuku, ikiwa na maana kwamba kuku mmoja kuwa na kabila moja au zaidi kwa mara moja. Hivyo aina za kuku zifuatazo zinaweza kutambuliwa kama ndiyo kabila za kuku wa Asili kulingana na maumbile yao na maeneo wanakotoka.

(i) **Kuchi**

Ni kuku wakubwa kwa umbo, warefu na wenye kusimama mgongo ukiwa wima. Kuchi wana manyoya machache mwilini hasa kifuani, wana mdomo mfupi na panga/vilemba vyao ni vidogo. Majogoo huwa na wastani wa uzito wa kilo 3.5 na mitetea kilo 2. Mayai ya kuchi yana uzito wa wastani wa gramu 45. Kuku hawa wanapatikana kwa wingi maeneo ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na Zanzibar. Kuku hawa ni wazuri kwa nyama.



*Kuku wa Asili aina ya Kuchi.*

(ii) **Umbo la Kati**

Kuku hawa ndiyo hasa wanaoitwa kuku wa kienyeji (wa kawaida). Uzito - Majogoo wastani kilo 1.9, Mitetea wastani wa kilo 1.1, Mayai yana wastani wa gramu 43. Kuku hawa hupatikana sehemu zote za nchi na rangi ya manyoya yao ni mchanganyiko. Kwa kawaida wanaonekana kuwa na uzito mdogo kwa sababu kuna tofauti kubwa sana baina ya ukubwa wa kundi la aina hii. Utafiti umeonyesha kwamba kuku hawa hukua upesi na pia hupata kinga upesi baada ya kuwachanja dhidi ya ugonjwa wa Mdondo *(New Castle disease).*

(iii) **Ching'wekwe**

Kuku hawa hutaga mayai mengi sana kuliko aina nyingine ya kuku wa Asili waliopo Tanzania kwa hiyo wanafaa sana kwa biashara ya mayai. Kuku hawa wenye umbo dogo na wafupi hupatikana zaidi sehemu ya Chakwale mkoani Morogoro na pia sehemu za Umasaini. Uzito – Majogoo wastani wa kilo 1.6 na Mitetea wastani wa kilo 1.2. Mayai yana wastani wa gramu 37.

(iv) **Singamagazi**

Kuku hawa wana utambulisho maalum kutokana na rangi zao, kwani majogoo huwa na rangi ya moto na mitetea huwa na rangi ya nyuki. Ni aina ya kuku wakubwa wa asili wanaopatikana zaidi maeneo ya Tabora. Uzito - Majogoo wastani wa kilo 2.9 na Mitetea wastani wa kilo 2.0. Mayai yana

wastani wa gramu 56. Kuku hawa ni mbegu nzuri kwa uzalishaji wa mayai na nyama.

(v) **Mbeya**



Mfugaji wa Kuku wa Asili akiwa amebeba kuku aina ya Mbeya.

Rangi ya manyoya ya kuku hawa ni nyeusi au bluu iliyokolea. Uwezo wao wa kuatamia mayai na kuangua ni mdogo sana ukilinganisha na kuku wengine. Uzito – Majogoo wastani wa kilo 3 na Mitetea kilo 2.0. Mayai yana wastani wa gramu 49. Kuku hawa wanapatikana Ileje mkoani Mbeya, lakini asili haswa ya kuku hawa ni nchi jirani ya Malawi. Hata hivyo, si wa kienyeji asilia bali wana damu ya kuku wa kisasa aina ya *'Black Australorp'.*

(vi) **Pemba**

Wana maumbo ya wastani na miili yao ni myembamba. Kuku hawa wanapatikana maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Pemba. Rangi ya manyoya yao ni mchanganyiko, panga na vilemba vyao ni vidogo. Uzito - Majogoo wastani wa kilo 1.5 na Mitetea wastani wa kilo 1.0. Mayai yana wastani wa gramu 42.

(vii) **Unguja**

Hawana tofauti kubwa sana na wale wa Pemba isipokuwa panga / vilemba vyao ni mchanganyiko kati ya vidogo na vikubwa. Kuku hawa wanapatikana maeneo mbalimbali ya kisiwa cha unguja. Uzito – Majogoo wastani kilo 1.6 na Mitetea wastani wa kilo 1.2. Mayai yana wastani wa gramu 42.

Kuku hawa wa Unguja na Pemba wanashabihiana sana na Kuchi isipokuwa kuku hawa (Unguja na Pemba) ni wadogo.

(vii) **Aina nyingine**

Kuna aina nyingine za kuku wa asili wanaotambuliwa kwa muonekano wao. Kuku hawa hupatikana sehemu mbalimbali za Tanzania lakini bado hawajaweza kuainishwa vizuri ili kuweza kutambua sifa zao. Kuku hawa ni pamoja na:

- ***Kishingo*** – Kuku wasio na manyoya shingoni.
- ***Njachama au Nungunungu*** – wenye manyoya yaliyosimama.
- ***Kibwenzi*** – Wenye manyoya mengi kichwani.

- ***Kibutu*** – wasio na manyoya mkiani.

**Muhimu: Mkulima akifanya uchaguzi vizuri kutoka katika kuku wa Asili na kutoa matunzo mazuri kwa hao kuku waliochaguliwa, hakika anaweza kupata kuku walio bora wenye uzito wa kutosha na  wenye kutaga mayai mengi na makubwa.**

## Mada ya 3: Mifumo ya Ufugaji Kuku wa Asili

Ipo mifumo ya aina 3 ya ufugaji wa kuku wa Asili inayotumika nchini Tanzania. Mifumo hiyo ni *Ufugaji Huria, Ufugaji Nusu Huria* na *Ufugaji wa Ndani.* Kila mfumo una faida na hasara zake. Ni vyema mfugaji kuijua mifumo yote na kisha kuchagua anaoona ni bora kulingana na mazingira yake. Hata hivyo, katika kufanya uteuzi ni vyema kutilia maanani mfumo wenye faida zaidi na kuepuka mfumo wenye hasara nyingi.

### 1. Ufugaji Huria:

Katika mfumo huu, kuku huachiwa kuanzia asubuhi wakitembea kujitafutia wenyewe chakula na maji na kufungiwa kwenye vibanda visivyo rasmi wakati wa usiku. Huu ni mfumo rahisi lakini si mzuri kwa mfugaji wa kuku wengi kwani atahitaji eneo kubwa la ardhi.

**Faida Zake:**

i. Gharama ndogo za ujenzi wa banda.

ii. Gharama za chakula hupungua kwani kuku huokota wadudu na kula baadhi ya majani.

iii. Gharama za kujenga uzio hazihitajiki.



*Banda la Ufugaji Huria*

**Hasara zake:**

i. Uwezekano mkubwa wa kuku kuliwa na vicheche, mwewe na wanyama wengine, kuibwa mitaani au kukanyagwa na magari.

ii. Kuku hutaga popote na upotevu wa mayai ni mkubwa.

iii. Kuna usimamizi hafifu wa kundi la kuku.

iv. Ni rahisi kuku kuambukizwa magonjwa.

v. Utagaji unakuwa si mzuri kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa.

vi. Uwekaji wa kumbukumbu si mzuri na mara nyingi kumbukumbu si sahihi.

vii. Si rahisi kugundua kuku wagonjwa na utoaji wa tiba na kinga ni mgumu.

viii. Vifaranga wengi hufa na kupotea.

**Uboreshaji wa mfumo huu:**

i. Kuku wajengewe banda kwa ajili ya kulala nyakati za usiku na liwasaidie wakati mwingine wowote hali ya hewa inapokuwa sio nzuri.

ii. Kuku wapatiwe chakula cha ziada na maji.

iii. Kuku waandaliwe viota vya kutagia.

iv. Kuku 100 watumie eneo la ardhi la ekari moja.

**2. Ufugaji Nusu Huria:**

Katika mfumo huu kuku hujengewa banda rasmi na banda hilo huzungushiwa wigo (uzio) au wigo huo hujengwa kwa mbele, ambapo kuku hulala ndani ya banda nyakati za usiku na kushinda nje ya banda (ndani ya wigo) nyakati za mchana wakila chakula na kunywa maji humo. Mfumo huu ni ghali kiasi kuliko mfumo huria, lakini huweza kumpatia mfugaji tija haraka sana.

**Faida zake:**


i. Sehemu ndogo ya kufugia hutumika kuliko ufugaji huria.

ii. Utunzaji wa kuku ni rahisi ukilinganisha na ule wa huria.

iii. Ni rahisi kutibu na kukinga maradhi ya milipuko kama mdondo *(New Castle Disease).*

iv. Upotevu wa kuku na mayai ni mdogo ukilinganisha na mfumo Huria.

v. Uwekaji wa kumbukumbu ni rahisi.



*Mchoro: Mfano wa Banda la mfumo wa Nusu Huria.*

**Hasara zake:**

i. Unahitaji gharama za banda na uzio.

ii. Gharama za chakula zitakuwa kubwa ukilinganisha na ufugaji huria.

iii. Matumizi ya muda mrefu ya eneo husika laweza kuwa na minyoo au vimelea vingine vyovyote vya magonjwa.

**Uboreshaji wa mfumo huu:**


i. Fanya usafi wa eneo husika na banda kila siku.

ii. Ikiwezekana kuwe na mzunguko wa kutumia eneo hilo.

**Muhimu: Ili mfugaji aweze kupata tija na mafanikio katika ufugaji wa kuku wa Asili anashauriwa atumie mfumo huu.**

**3. Ufugaji wa Ndani:**

Katika mfumo huu, kuku hujengewa banda rasmi na hufugwa wakiwa ndani huku wakipatiwa chakula, maji na kufanyiwa huduma nyingine muhimu wakiwa humo ndani kwa muda wote wa maisha yao. Kwa mfumo huu, kuku huwekwa kwenye mabanda ambayo sakafu hufunikwa kwa matandiko ya makapi ya mpunga, takataka za mbao (takataka za randa), maganda ya karanga au majani makavu yaliyokatwakatwa.



*Banda la Ufugaji wa Ndani*

**Faida zake:**

i. Mfumo huu unahitaji eneo dogo la kufugia hivyo ni mzuri kwenye maeneo yenye uhaba wa ardhi.

ii. Uangalizi wa kuku ni mzuri na rahisi.

iii. Ni rahisi kuhakikisha ubora wa chakula.

iv. Hakuna haja ya kufagia vinyesi vya kuku kila siku.

v. Kuku wanakingwa na hali mbaya ya hewa na maadui wengine.

vi. Ni rahisi kukinga na kutibu maradhi ya kuku.
vii. Uwekaji wa kumbukumbu ni rahisi.
viii. Ni rahisi kudhibiti upotevu wa kuku, vifaranga na mayai.

**Hasara zake:**

i. Uwezekano wa kuku kudonoana na kula mayai ni mkubwa kama utunzaji utakuwa duni.
ii. Uwezekano wa kuku kuatamia mayai bila mpangilio ni mkubwa.
iii. Ujenzi wa mabanda na ulishaji una gharama kubwa.
iv. Mahitaji makubwa ya nguvu kazi.
v. Kuku watakosa mionzi ya jua ambayo ni muhimu kwa kutoa vitamini D.
vi. Ni rahisi ugonjwa kuenea haraka unapoingia kwenye kundi.

**Muhimu: Kutokana na uwezo mdogo wa uzalishaji kimaumbile, kuku wa asili hawataleta tija kwa mfugaji iwapo atatumia mfumo huu.**

**Uboreshaji wa mfumo huu:**

i. Hakikisha utunzaji mzuri wa matandiko na usafi wa banda ili kupunguza unyevunyevu na joto kali ndani ya banda.
ii. Kuku wawe na nafasi ya kutosha, mita mraba moja hutosha kuku 5-8.

## Mada ya 4: Maandalizi ya Ufugaji Kuku wa Asili


Ili uweze kufuga kuku wa Asili kwa faida, ni vyema kufanya maandalizi ya awali yatakayokuwezesha kuzalisha kuku walio bora. Maandalizi hayo yanajumuisha utayarishaji wa banda kulingana na idadi ya kuku utakaofuga, uchaguzi wa kuku bora na uandaaji wa vifaa vya kulishia au kutagia na uwiano wa kuku ndani ya banda.

### 1. Banda bora:

Ni muhimu kuwajengea kuku banda bora ili wapate kujikinga na mvua, baridi, wezi na wanyama. Banda la kuku linaweza likajengwa kando kando au nyuma ya nyumba ya kuishi. Eneo linapojengwa banda la kuku pawe:

- Panafikika kwa urahisi.
- Pasituamishe maji.
- Pasiwe pa mwelekeo wa upepo mkali.

Banda la kuku linaweza kujengwa kwa kutumia raslimali za misitu zinazopatikana kwa urahisi kwenye eneo husika. Vifaa muhimu katika ujenzi wa banda ni pamoja na miti, nyasi, mabati, makuti, fito, udongo, mabanzi, saruji na vifaa vingine mbalimbali vya ujenzi.




*Mchoro: Banda la Kuku wa Asili kwa ufugaji wa Nusu Huria (kwa kuku 20 wakubwa na 120 wanaokua)*

**2. Sifa za banda bora la kuku:**

- Liwe na paa imara lisilovuja.
- Kuta zisiwe na nyufa kama umetumia tofali (zisilibwe au zipigwe lipu) kwani nyufa ni maficho ya wadudu kama viroboto, utitiri, chawa nk.
- Sakafu isiwe na nyufa au mipasuko.
- Liwe na madirisha ya kutosha kupitisha hewa.
- Liwe na uwezo wa kuingia mtu wa kufanya usafi na huduma nyingine muhimu.
- Liwe na ukubwa (nafasi) unaolingana na idadi ya wastani wa kuku 10-15 kwa mita moja mraba kwa kuku wanaofugwa huria, ili wawe na nafasi ya kulala tu wakati wa usiku. Ila kwa kuku wanaofugwa kwa mfumo wa nusu ndani nusu nje wanastahili eneo la mita moja mraba kwa kuku 4 - 5 ili kuruhusu nafasi ya vyombo vya chakula na maji.

**3. Kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi:**

Mafanikio zaidi katika kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi yatapatikana iwapo uchaguzi na uchambuzi wa kuku wanaozaliwa utafanywa mara kwa mara. Sababu kubwa ya kufanya uchaguzi ni kupata kundi la kuku litakalofaa kwa sifa zote katika uzalishaji. Sifa hizo ni pamoja na kupevuka haraka, kutaga mayai mengi, kuwa na uzito mkubwa na nyama nyingi kwa umri mdogo. Ufugaji bora utazingatia kuchagua kuku wenye sifa nzuri na kuwaacha waendelee na uzalishaji na wanaosalia wauzwe au waliwe.

Vilevile kuku wa Asili wanaweza kuboreshwa zaidi kwa kutumia majogoo ya kisasa kama vile *Rhode Island Red-RIR* ili kupata kuku wanaokua haraka wenye uzito mkubwa na kutaga mayai mengi zaidi.



*Jogoo aina ya Rhode Island Red*

***Sifa za kuzingatia wakati wa kuchagua mitetea:***

Wawe na:

- Umbile kubwa.
- Uwezo wa kutaga wakiwa na umri mdogo (miezi 6).
- Uwezo wa kustahimili magonjwa.
- Uwezo wa kukua haraka.
- Uwezo wa kutaga mayai mengi {zaidi ya 15 kwa mtago mmoja (*clutch)*}.
- Uwezo wa kuatamia na kuangua vifaranga wengi na kuwalea.

***Sifa za kuzingatia wakati wa kuchagua majogoo:***

Jogoo bora, awe na:

- Umbo kubwa.
- Miguu imara na yenye nguvu.
- Kucha fupi.
- Mwenye nguvu.
- Machachari.
- Upanga/kilemba kikubwa.
- Uwezo wa kuitia chakula mitetea.
- Tabia ya kupenda vifaranga.

**Njia zitumikazo katika kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi:**

- Kwa kuangalia kuku wenyewe kulingana na sifa zilizotajwa hapo juu.
- Kwa kufuatilia kumbukumbu za wazazi wa kuku unaotaka kuwachagua.
- Kwa kuangalia kumbukumbu za familia (wazazi, kaka na dada).

**Wakati muafaka wa kuchagua kuku wa kuendeleza kizazi:**

- Mara tu wakitotolewa.
- Wakati wa ukuaji.
- Zoezi endelevu.
- Uzalishaji ukishuka chini ya asilimia 50.
- Wakati kuku wanapoangusha manyoya.

**Faida ya kuondoa kuku wasiofaa kwenye kundi:**

- Inasaidia kuongeza uzalishaji wa mayai.

- Inapunguza kulisha kuku ambao uzalishaji wake ni hafifu.
- Inapunguza uenezaji wa magonjwa ya kuku.
- Huongeza nafasi zaidi kwa kuku wazuri kwenye banda.
- Uwezekano wa kuuza kuku kama hao ni mkubwa kabla hawajafa.

**Umri wa kupevuka:**

- Mitetea huanza kutaga wakiwa na umri wa miezi 6 - 8.
- Jogoo huanza kupanda akiwa na umri wa miezi 7 lakini mbegu zake huwa bado kukomaa. Hutoa mbegu zilizokomaa anapofikia umri wa miezi 10.

**Muhimu: Ni vizuri jogoo atumike kwa miaka mitatu tu ili kuepuka mchanganyiko wa damu kwa wenye nasaba moja kwani kufanya hivyo husababisha uzalishaji duni. Kama umeamua kufuga kuku wa mzao wa kwanza (F1) ni vyema kuwapandisha mitetea hao (F1) kwa majogoo ya asili ili kuendeleza damu ya asili.**

**Uwiano wa mitetea na majogoo:**

Ili kudumisha amani katika kundi la kuku, na ili kupata mayai yenye mbegu ya jogoo ambayo yana uwezo wa kutoa vifaranga ni muhimu kuangalia uwiano kati ya mitetea na majogoo. Sio sahihi kuweka mitetea wengi kwa majogoo wachache na majogoo wengi kwa mitetea wachache. Uwiano unaokubalika ni wastani wa jogoo mmoja kwa mitetea kumi hadi kumi na mbili {1: 10-12}.

**4. Fuga kuku upate faida kwa kuzingatia:**

Elimu na Ushauri kutoka kwa mtaalamu wa mifugo na kutimiza yafutayo:

- Chanjo ya mdondo kila baada ya miezi 3.
- Chanjo ya ndui mara 2 kwa mwaka.
- Zuia viroboto, utitiri na minyoo.
- Chagua mayai bora kwa ajili ya kuatamiza.
- Panga kuuza kuku kwa makundi uongeze kipato.
- Boresha lishe ya familia kwa kula mayai na kuku.
- Gawa mapato yatokanayo na ufugaji wa kuku kwa matumizi yako (33%), maendeleo ya mradi (33%), na akiba (33%).

## Mada ya 5: Vifaa Muhimu Ndani ya Banda la Kuku

Ufugaji wenye tija unahitaji kuhakikisha kuwa vifaa muhimu vinakuwemo ndani ya banda kwa uwiano unaotakiwa kati ya kuku na vifaa hivyo. Vifaa hivyo ni pamoja na:


1. Vyombo vya Chakula
2. Vyombo vya Maji
3. Viota
4. Vichanja, na
5. Matandiko


**1. Vyombo vya Chakula:**

Ni muhimu kuwa na vyombo vya kutosha ili kuwawezesha kuku kula pasipo kusongamana. Vyombo hivyo lazima viwe safi na bora ili kuongeza ufanisi katika kufuga kuku.

Vyombo vinavyotakiwa ni vile vinavyoweza kuzuia upotevu wa chakula. Kuku wasipewe nafasi ya kuchakura ndani ya vyombo hivyo ili kupunguza kupotea kwa chakula. Unaweza kuzuia upotevu huo kwa kuweka vyombo hivyo juu ya mawe, gogo au kuvining'iniza.

Vyombo vya chakula vinaweza kutengenezwa na mfugaji mwenyewe kwa kutumia vifaa mbali mbali vilivyomo katika mazingira yake na si lazima vile vilivyotengenezwa viwandani. Baadhi ya vitu vinavyoweza kutumika ni pamoja na kipande cha gurudumu la gari lililotumika, gogo lililochimbwa kati na kadhalika.





*Mchoro: Mfano wa uwekaji wa vyombo vya chakula vikiwa vimening'inia.*


**Faida za kutumia vyombo bora:**

- Huzuia kuchafuka kwa chakula.
- Huzuia kupotea kwa chakula.
- Hupunguza uwezekano wa kuku kuambukizwa magonjwa kama vile *coccidiosis*, minyoo n.k.

**2. Vyombo Vya Maji:**

Vyombo vya maji ni muhimu sana kwa kuku pasipo kuangalia wanafugwa kwa mtindo gani. Maji safi ni muhimu sana kwa kuku kwani huwafanya kuku kuwa na afya bora na kuongeza ufanisi katika utagaji wa mayai. Ni vyema kutumia vyombo vya maji ambavyo ni rahisi kuvifanyia usafi, visivyo na uwezekano wa kumwaga maji hovyo.

Vyombo vya maji ni vyema vikaning'inizwa ili kuwawezesha kuku kunywa maji kwa urahisi na pia kuzuia maji kuchafuliwa na kumwagwa kwa urahisi.





*Baadhi ya vyombo vya maji.*

**3. Viota:**

Ni vyema kuwepo na sehemu maalumu ya kutagia ndani ya banda la kuku. Sehemu hii inatakiwa kuwa tulivu, faragha na yenye mwanga hafifu.

Kutokuwepo kwa viota husababisha kuku kutaga mayai hovyo na kupotea kwa mayai mengi pasipo kujua na uanguaji huwa mbaya, hivyo kupunguza uzalishaji wa kuku na kurudisha nyuma shughuli ya uzalishaji.

Kiota kinatakiwa kuwa na nafasi nzuri ya kumuwezesha kuku kuenea na kuweza kujigeuza. Kwa wastani kiota kinatakiwa kuwa na urefu wa sentimita 35, upana wa sentimita 35 na kina cha sentimita 35. Pia kiota kiwekwe juu kwa sentimita 50 toka sakafuni ili kumfanya kuku



*Mfano wa viota vya kuku.*


kujisikia salama zaidi.

Viota vinatakiwa viandaliwe mapema kulingana na idadi ya makoo uliyo nayo. Ndani ya kila kiota utatakiwa kuweka matandiko ili kuongeza joto na usalama wa mayai. Idadi ya viota iwe robo tatu ya idadi ya kuku waliofikia umri wa kutaga.

**4. Vichanja vya Kupumzikia na Kulala:**

Kwa asili kuku hupendelea zaidi kulala juu kama kwenye miti kwani hujisikia kuwa na usalama zaidi kuliko wakiwa katika sehemu isiyo na mahali pa kudanda. Hivyo ili kuwafanya kuku wajisikie vizuri hapana budi kuwatengenezea vichanja sehemu ya nje wanaposhinda na kula chakula, na pia ndani ya banda ili kuwawezesha kulala vizuri nyakati za usiku.

Kwa kawaida vichanja vinatakiwa vitengenezwe kwa urefu wa mita moja toka ardhini. Vijiti vya juu vyapaswa kuwa vya duara vyenye kipenyo kinachowezesha miguu ya kuku kuzunguka vizuri na kubana.




*Mfano wa kuku wakiwa wamedanda kwenye kichanja.*



*Vijiti vya juu vyapaswa kuwa vya duara vyenye kipenyo kinachowezesha miguu ya kuku kuzunguka vizuri na kubana.*

**Faida za kutumia vichanja:**

i. Huzuia kuku kulala hovyo ndani ya viota.

ii. Hupunguza mashambulizi ya wadudu kama viroboto, utitiri na wadudu wengineo wanaoweza kuwa kwenye matandiko.

**5. Uwekaji wa Matandiko:**

Matandiko yanaweza kuwa ni maranda ya mbao, makapi ya mpunga na kahawa n.k. Matandiko husaidia sana kufyonza unyevunyevu toka ardhini na kutoka kwenye kinyesi. Pia huzuia maradhi

yatokanayo na baridi na unyevunyevu hususani kwa vifaranga. Utahitaji matandiko yenye ujazo wa unene wa sentimeta 5 hadi 10 ili kuwawezesha kuku wako kuwa katika hali iliyo nzuri. Mara unapoona dalili za matandiko kulowa inabidi kuyaondoa mara moja kwani ni rahisi kuoza na kuleta madhara kwa kuku. Inashauriwa kubadili matandiko ndani ya banda la kuku kila inapobidi.

## Mada ya 6: Vyakula na Ulishaji wa Kuku wa Asili

Ili kuku waweze kukua vizuri na kutoa mazao mengi na bora wanahitaji chakula chenye virutubisho vyote muhimu vinavyojumuisha makundi matano (5) kama ifuatavyo:

i. Protini

ii. Wanga

iii. Vitamini na

iv. Madini

v. Maji

Kwa ujumla kuku wote wanahitaji chakula chenye mchanganyiko kamili ili waweze kuwa na afya nzuri. Hata hivyo, aina ya mchanganyiko wa chakula inatofautiana kutoka kundi moja la kuku hadi jingine. Kwa mfano, vifaranga huitaji virutubisho aina ya protini kwa wingi kuliko kuku wakubwa ili waweze kukua vizuri na kuku wazazi pia huitaji virutubisho kuweza kujiimarisha na kutaga mayai mengi zaidi. *Jedwali namba 1* linaonyesha mchanganyko wa chakula ambao mfugaji anaweza kuandaa kwa ajili ya kuku wake, kwa ujazo wa kilo 50.

Unaweza kuamua kuchanganya kilo 50 zaidi au chini ya hapo ya mchanganyiko huu kulingana na kiasi utakachohitaji kwa kugawanya kiasi cha uwiano kutokana na uwezo wako au idadi ya kuku unaowafuga.

***Jedwali na. 1: Mchanganyiko wa chakula kwa makundi mbalimbali ya kuku kwa ujazo wa kilo 50***

| Na. | Aina ya Chakula | Mchanganyiko (katika kilogramu) kwa ajili ya: | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Vifaranga | Kuku Wanaokua | Kuku Wazazi | Kuku Wengineo |
| 1. | Mahindi Yaliyobarazwa | 8 | 8 | 8 | 10 |
| 2. | Pumba za Mahindi | 20 | 20 | 20 | 25 |
| 3. | Mashudu ya Alizeti | 8 | 7 | 10 | 6 |
| 4. | Unga wa Dagaa/Samaki | 6 | 6 | 3.5 | 3 |
| 5. | Unga wa Mifupa | 0.75 | 1.5 | 3 | 1 |
| 6. | Chokaa ya Mifugo | 1.75 | 2 | 4 | 4 |
| 7. | Chumvi ya Mezani | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| 8. | Soya Iliyobarazwa | 3 | 3 | - | - |
| 9. | Unga wa Damu | 1 | 1 | - | - |
| 10. | Premix | 1 | 1 | - | 0.5 |
| 11. | Egg Booster | - | - | 1 | - |
| **Jumla** | | **50** | **50** | **50** | **50** |

**Baadhi ya vyakula vyenye asili zifuatazo pia vinafaa kulisha kuku:**

i. **Mizizi** - Mihogo, Viazi vitamu, Mbatata, Magimbi.

ii. **Nafaka** - Mahindi, Mpunga, Mtama, Ulezi, Pumba za nafaka zote.

iii. **Mboga** - Jamii ya mikunde, mboga za majani, nyanya, pilipili, majani laini ya ukoka, majani ya mapapai, lukina, milonge na kisamvu.

iv. **Matunda** - kama vile Mapapai, Maembe na Matikiti maji.

v. **Mashudu** - Kama vile Karanga, Ufuta, Mashudu ya pamba, Alizeti, Soya, Machicha ya nazi.

vi. **Wadudu mbalimbali** - Panzi, Mchwa, Minyoo ya ardhini, Mende, Funza, Kumbikumbi n.k.

**Muhimu: Hakikisha kuku wanapata maji ya kunywa ya kutosha, ni vizuri kuku wanaofugwa huria wawekewe maji ya kunywa chini ya vivuli vya miti muda wote nyakati za mchana.**

Vingi ya vyakula vilivyotajwa hapo juu hupatikana kwa wingi zaidi wakati wa mvua au mara tu baada ya mavuno. Kwa kawaida baada ya kipindi hiki hutokea upungufu mkubwa wa vyakula hivi. Hali hii huchangia katika kupunguza kasi ya ukuaji na utagaji wa kuku. Kwahiyo ni muhimu kuku wakapewa chakula cha ziada ili waweze kuzalisha ipasavyo.

Kuku aliyepevuka anayefugwa huria anahitaji angalau gramu 80 za chakula cha ziada kwa siku. Ni vyema chakula cha ziada kitokane na vyakula vinavyopatikana kwa urahisi katika mazingira husika na ambacho hakina ushindani na mfugaji.

Hakikisha wakati wote chakula cha kuku kinaandaliwa na kuhifadhiwa kikiwa kikavu (kisilowe maji) ili kisiharibike kwani chakula kilichovunda kinaweza kuleta madhara kwa kuku. Pia kisitengenezwe chakula kingi kwa wakati mmoja na kukaa muda mrefu bila kutumika. Hali hiyo hufanya chakula kipoteze ubora wake.

***Jedwali na. 2: Kiwango cha Ulishaji kwa Umri:***

| Umri kwa wiki | Kiwango cha kulisha kuku kwa siku (gramu) |
|---|---|
| 1 | 12 - 15 |
| 2 | 15- 21 |
| 3 | 21 - 35 |
| 4 - 7 | 35 - 50 |
| 8 - 15 | 55 - 60 |
| 16 - 27 | 65 - 80 |

Mfano wa kiasi cha chakula cha ziada kwa kulisha kwa siku kuku wa kienyeji watano na vifaranga kumi na tano:

| | |
|---|---|
| Jogoo mmoja - | 1 x 65 gm = 65 gm |
| Mitetea - | 4 x 65 gm = 260 gm |
| Vifaranga - | 15 x 25 gm = 375 gm |
| | **Jumla 700 gm** |

**Mafunzo kwa vitendo:**
Washiriki wachanganye chakula cha kuku kwa kufuata vipimo walivyoelekezwa kwenye nadharia.

# Mada ya 7: Utagaji, Uatamiaji na Uanguaji wa Vifaranga

Kwa kawaida kuku wa Asili anapofikia umri kati ya miezi sita hadi minane huanza kutoa mlio (kutetea) unaoashiria yuko karibu kuanza kutaga mayai. Hivyo ni vyema viota viandaliwe mapema kuku wakiwa na umri wa miezi minne au mitano ili waanze kuvizoea.

Kuku anapoanza kutaga, akifikisha mayai matatu, mfugaji anashauriwa kuondoa kila yai linalozidi na kuacha hayo hayo matatu kila siku.Hakikisha kila yai linalokusanywa linawekwa alama ya tarehe au namba kwa kutumia kalamu ya risasi au penseli ili kumfanya kuku aendelee kutaga kwa lengo la kufikisha mayai 15 – 20. Mayai yanayoondolewa yahifadhiwe kwenye chombo kikavu chenye kupitisha hewa kama *trei* au boksi lililowekwa mchanga au hata chungu kilichojazwa mchanga.

**Fuata utaratibu ufuatao kuhifadhi mayai:**

- Sehemu ya yai iliyochongoka iwe chini na pana iwe juu.
- Hifadhi sehemu yenye kupitisha hewa ya kutosha na isiyokuwa na joto.
- Mayai yasikae kwenye hifadhi hiyo zaidi ya wiki mbili toka siku yalipotagwa.

**Sifa za mayai ya kuatamiwa:**

Ni vizuri kuchagua mayai ya kuatamia ili mayai yasiyofaa yaweze kuuzwa au kutumika nyumbani kwa chakula. Sifa za mayai mazuri ya kuatamiwa ni kama ifuatavyo:

- Yawe masafi na wala yasisafishwe au kufutwa na kitambaa chenye maji kama ni machafu.
- Yasiwe na nyufa.
- Yatokane na kuku aliyepandwa na jogoo.
- Yawe na ukubwa wa wastani kulingana na umbile au aina ya kuku.
- Yasiwe ya mviringo kama mpira pia yasiwe na ncha kali.
- Yasiwe yamekaa muda mrefu zaidi ya wiki mbili toka siku yalipotagwa.
- Yasiwe yaliyohifadhiwa kwenye sehemu yenye joto.



*Mchoro: Mayai yaliyohifadhiwa ndani ya trei.*

**Njia za uatamiaji na uanguaji:**

Kuna njia mbili za uatamiaji na uanguaji, ambazo ni:

1. Uatamiaji na uanguaji wa kubuni.
2. Uatamiaji na uanguaji wa asili.

Njia yoyote utakayochagua inahitaji maandalizi ya kina, hususani ya uchambuzi wa mayai yatakayoweza kutotolewa.

**1. Uanguaji wa Kubuni:**

Uanguaji wa kubuni ni kwamba mashine za kutotoleshea vifaranga *(incubators)* hutumika kuangua mayai mengi kwa wakati mmoja. Wafugaji wadogowadogo huwa na mashine za kutotolea vifaranga ambavyo huweza kuangua kati ya mayai 50 na 500. Mashine zinazotumika kutotoleshea vifaranga vya kuku wa kisasa zinaweza pia kutumika kutotoleshea vifaranga vya kuku wa kienyeji, aidha zipo mashine zinazotengenezwa hapa nchini na nje ya nchi.



*Picha inayoonyesha aina mojawapo ya incubator*

**Faida za kutumia mashine kutotoleshea vifaranga:**

- Vifaranga huanguliwa kwa wingi na wakati mmoja
- Vifaranga waliototolewa wakati mmoja hukua kwa pamoja na kuweza kuuzwa pamoja, hivyo hurahisisha uzalishaji.
- Kuku walionyang’anywa mayai ili yaanguliwe kwa mashine huanza kutaga tena mayai mapema hivyo hutaga mayai mengi kwa mwaka.

**Changamoto za utumiaji wa mashine za kutotoleshea vifaranga:**

- Utaalam wa kutumia mashine huhitajika.
- Muda mwingi hutumika kufuatilia mwenendo wa mashine.
- Nishati ya uhakika huhitajika ama sivyo utotoaji hautakuwa mzuri.

**2. Uanguaji wa asili:**

Uanguaji wa asili ndiyo unaotumika kwa kuku wetu wa Asili ambapo kuku hutaga mayai na baadaye huatamia na hatimaye kutotoa vifaranga. Inashauriwa kumuwekea kuku mayai ya kuatamia kati ya 12 na 15 kwa wakati mmoja kufuatana na umbile la kuku.

**Faida za uanguaji wa Asili wa vifaranga:**

- Gharama huwa ni kidogo.
- Mfugaji hahitaji ujuzi maalumu katika kufanya shughuli hii.
- Huhitaji kurekebisha joto, unyevunyevu, hali ya hewa na hata kugeuza mayai kama inavyofanyika kwenye mashine.
- Kutohitaji nguvu kazi yoyote.

**Kuchagua mtetea anayeweza kuatamia mayai yasiyokuwa yake:**

Yaweza kutokea baadhi ya kuku wakawa watagaji wazuri wa mayai lakini hawapendi kuatamia. Katika hali hiyo ni vyema wakachaguliwa kuku (mitetea) wengine ili kuatamia mayai yao kwa uanguaji mzuri.

Utaratibu ufuatao utatumika:

- Tafuta mtetea aliyefikia umri wa kutaga au kuku aliyekwishawahi kutotoa.
- Tafuta mawe matatu ya mviringo au viazi mbatata vya ukubwa wa yai au vibao vilivyochongwa kwa umbile la yai (mayai bandia).
- Muwekee kuku huyo mayai bandia yasiyopungua matatu kwenye kiota wakati wa usiku na umfungie humo usiku kucha hadi asubuhi na ukimuona anaendelea kuatamia basi usiku unaofuata toa mayai bandia na umuwekee mayai halisi.
- Weka mayai kwenye kiota huku mikono yako ikiwa imepakwa majivu ili kuepuka kuwa na harufu kwani kuku anaweza kuyasusa.

**Kuwatayarisha kuku wa kuatamia:**

Kuku wanaotazamiwa kuatamia ni lazima wachunguzwe kwa makini kabla ya kuatamia ili kuhakikisha kwamba hawana chawa, utitiri au viroboto. Kuwepo kwa wadudu hao kutawafanya kuku wakose raha na wasitulie kwenye viota vyao, matokeo yake ni kuanguliwa kwa vifaranga wachache. Ili kuua au kuzuia wadudu hawa, fanya yafuatayo:

- Toa matandiko *(litter)* ndani ya kiota.
- Nyunyiza dawa ya kuua wadudu (viroboto, utitiri nk.) ndani ya kiota.
- Pia mnyunyizie dawa kuku anayetarajiwa kuatamia.



*Mfano wa viota ambamo kuku huatamia mayai.*

**Kuwafanya kuku wengi kutotoa kwa wakati mmoja:**

Kuna uwezekano mkubwa tu wa kuweza kuwandaa kuku na kuweza kutotoa kwa siku moja. Njia ni rahisi na inaweza kuongeza tija katika ufugaji wa kuku wa Asili. Ili uweze kutotolesha kuku kwa wakati mmoja fanya yafuatayo:

- Kuku anapotaga kila siku weka alama kila yai linalotagwa aidha namba au tarehe kulingana na siku aliyotaga.
- Yanapofika mayai matatu yaondoe na muwekee mayai bandia na huku ukiendelea kukusanya na kuweka alama mayai yanayoendelea kutagwa kila siku.
- Mara kuku anapoanza kuatamia unaweza kumuongezea mayai bandia na kufikia 8 hadi10.
- Fanya hivyo kwa kila kuku anayetaga hadi utakapopata idadi inayoweza kukupatia vifaranga wengi kwa wakati mmoja.
- Chagua mayai ya kuatamia ukianza na yai la mwisho kutagwa. Wawekee kuku wote mayai siku moja kwa kuondoa mayai bandia na kuwawekea mayai ya kweli wakati wa usiku.
- Kuku huendelea kuatamia mpaka vifaranga vitoke hivyo ukimwekea mayai yasiyo na mbegu, atakaa hapo hapo kwa muda mrefu. Kwa kawaida kuku huatamia mayai kwa muda wa siku 21 kabla ya vifaranga kuanguliwa.

**Mbinu za kuzalisha kuku wengi kwa muda mfupi:**

Zoezi hili linawezekana iwapo uleaji wa vifaranga kwa njia ya kubuni litatumika kwani kuku mmoja anaweza kutotoa zaidi ya mara 7 kwa mwaka. Mafanikio ya mpango huu hupatikana kwa kuwanyang'anya kuku vifaranga vyao pale tu vinapototolewa (siku ya kwanza), na baada ya siku 14 kuku hurudia tena kutaga.

**Muhimu: Inashauriwa kutokuwa na majogoo wengi, hivyo yakupasa kudhibiti ongezeko la majogoo ndani ya banda. Waweza kufanya hivyo kwa kuhakikisha unayatambua mayai yanayoweza kuwa na mbegu ya jogoo mapema. Utafiti unaonyesha kuwa mayai membamba yenye ncha kali huwa na mbegu ya jogoo, hivyo yanaweza kuondolewa na kuliwa na familia au kuuzwa. Kwa utaratibu huo utakuwa umedhibiti ongezeko la majogoo ndani ya banda, isipokuwa kama unahitaji majogoo kwa ajii ya biashara waweza kuzalisha mengi zaidi.**

**Jedwali na. 3: Vifaranga wanaoweza kupatikana kutokana na kuku mmoja kwa mwaka mmoja:**

| Kitendo | Muda | Idadi | Wastani wa Kutotoa | Mzao wa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku | 15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***36*** | ***8*** | **Kwanza** | |
| Kupumzika<br>Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku<br>Siku | 14<br>15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***86*** | ***8*** | **Pili** | |
| Kupumzika<br>Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku<br>Siku | 14<br>15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***136*** | ***8*** | **Tatu** | |
| Kupumzika<br>Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku<br>Siku | 14<br>15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***186*** | ***8*** | **Nne** | |
| Kupumzika<br>Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku<br>Siku | 14<br>15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***236*** | ***8 x 5 = 40*** | **Tano** | ***Nusu ya vifaranga walioanguliwa siku ya 36 na ambao wanadhaniwa kuwa majike watakuwa wamepevuka na hivyo kuungana na mama yao kutaga na kutotoa vifaranga.*** |
| Kupumzika<br>Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku<br>Siku | 14<br>15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***286*** | ***8 x 9 = 72*** | **Sita** | ***Nusu ya vifaranga walioanguliwa siku ya 86 na ambao wanadhaniwa kuwa majike watakuwa wamepevuka na hivyo kuungana na mama yao kutaga na kutotoa vifaranga.*** |
| Kupumzika<br>Kutaga<br>Kuatamia | Siku<br>Siku<br>Siku | 14<br>15<br>21 | | | |
| | ***Siku*** | ***336*** | ***8 x 13 = 104*** | **Saba** | ***Nusu ya vifaranga walioanguliwa siku ya 136 na ambao wanadhaniwa kuwa majike watakuwa wamepevuka na hivyo kuungana na mama yao kutaga na kutotoa vifaranga.*** |
| **Jumla vifaranga** | | | **248** | | |

**Muhimu:**

- **Mayai ya kuatamia yasishikwe kwa mkono ulio wazi, kwani kwa kufanya hivyo yanaweza kupata harufu kama za mafuta ya kujipaka, mafuta ya taa au manukato. Hii hufanya kuku kuyakataa. Hivyo hakikisha umenawa mikono kwanza kisha jipake jivu mikononi, hapo ndipo unaweza kuyashika mayai.**
- **Kazi ya kumuandaa kuku anayetaka kuatamia ifanyike wakati wa usiku.**

**Jinsi ya kutambua mayai yaliyo na mbegu na yasiyo na mbegu:**

Ieleweke kuwa, si kila yai lina kiini cha mbegu. Kwani kuku anaweza kutaga yai hata pasipo kupandwa na jogoo, kwa hiyo ni muhimu kuwa makini ili kuhakikisha kuwa mayai yote yatakayoatamiwa yatatotolewa.

Mfugaji anaweza kutambua mayai yaliyo na mbegu na yasiyo na mbegu siku ya kumi tangu mayai kuatamiwa. Utatakiwa kutumia boksi lililotengenezwa kwa umbo la duara na kuliweka yai ndani yake au unaweza kulishika kwa mzunguko wake kwenye mkono wako na kuacha umbo la tundu chini ya mkono ili kufanya sehemu ya giza. Kwa kutumia kurunzi yenye mwanga mkali, mulika yai hilo toka upande wa wazi wa chini ya boksi au mkono. Zoezi hili lifanyike ndani ya chumba chenye kiza. Kwa kila yai litakalokuwa na kiza au nyuzi nyuzi kama mishipa hilo linaonyesha kuwa na mbegu na kwa yai litakalopitisha mwanga na kuonyesha rangi ya kawaida ya yai (njano) ina maana yai hilo halina mbegu. Mayai yasiyo na mbegu yanaweza kutumika kwa chakula cha familia au kuuzwa kwani bado ni bora na hayana madhara yoyote.

**Jedwali na. 4: Muda wa kuatamia mayai kwa ndege mbalimbali wafugwao:**

| Na. | Jina la Ndege | Muda/Siku |
|---|---|---|
| 1. | Kuku | 21 |
| 2. | Bata Mzinga | 28 |
| 3. | Bata Bukini | 28 |
| 4. | Bata *(Muscovy)* | 33-36 |
| 5. | Bata Maji *(Swan)* | 35 |
| 6. | Kanga | 28 |
| 7. | Kwale | 24 |
| 8. | Mbuni | 42 |
| 9 | Njiwa | 17 |
| 10. | Tausi | 26-28 |

**Mafunzo yafuatayo yanapaswa kufanywa kwa vitendo:**

- **Kutenganisha kuku (vijogoo na temba).**
- **Usafishaji wa mayai yaliyochafuka.**
- **Jinsi ya kutambua kuku watagao na wasiotaga.**

## Mada ya 8: Uleaji wa Vifaranga

Vifaranga ni hatua ya mwanzo ya ukuaji wa kuku, hivyo ni bora kuchukua tahadhari ili kuhakikisha ukuaji ulio bora wa vifaranga hao. Vifaranga vinahitaji malezi makini kuepusha magonjwa yanayoweza kusababisha vifo na hivyo kupunguza idadi ya kuku unaotarajia kuwa nao. Uhakika wa kuwa na kuku walio bora na wengi utategemea matunzo bora ya vifaranga utakayotoa tangu siku ya kwanza vifaranga vitotolewe. Vifo vingi vya vifaranga hutokea siku za mwanzoni vikishatotolewa. Hivyo basi, ili mfugaji aweze kupata tija na mafanikio kwa haraka kutokana na ufugaji wa kuku wa Asili, ni vyema kuhakikisha vifaranga vinalelewa katika mazingira mazuri toka siku ya kwanza.

Vifaranga huhitaji joto la ziada katika kipindi cha mwanzo cha ukuaji ambacho ni kati ya siku 1 hadi wiki ya nane. Hapa nchini, mara nyingi njia ya asili ya kutumia kuku wazazi hutumika kutoa joto la ziada kwa vifaranga kwa kipindi cha wastani wa siku 90.

Kuna mifumo (2) miwili ya uleaji wa vifaranga ambayo ni:

1. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili.
2. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni.

### 1. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili:

Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili ni ule uliozoeleka, ambapo kuku mwenyewe baada ya kutotoa hutembea na vifaranga vyake akivisaidia kutafuta chakula na kuvikumbatia kila baada ya muda fulani ili kuvipatia joto.

Mfumo wa asili umekuwa hauna tija kwa kusababisha ukuaji wa vifaranga kuwa duni na vingi kushambuliwa na wanyama na ndege na vingine kufa. Na vile vile mizunguko ya utagaji wa kuku kwa mwaka huwa michache. Kwa kutumia mfumo huu vifaranga hulelewa kwa takribani miezi (3) mitatu.

Kama utalea vifaranga kwa mfumo wa asili, basi ni vizuri kumtenga kuku mwenye vifaranga na kumuweka kwenye chumba cha pekee ili vifaranga visishambuliwe na kuku wengine hali kadhalika kuwalinda na wanyama na ndege wanaoshambulia vifaranga kama vile vicheche, mwewe na kunguru.

### 2. Uleaji wa vifaranga mfumo wa kubuni:

Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni ulikuwa unatumika zaidi kwa ufugaji kuku wa kisasa ambao hutotolewa kwa wingi sana, ambapo vifaranga huwekwa kwa pamoja kwenye chumba maalum na kupatiwa joto maalum, chakula pamoja na maji. Utaratibu huu pia unaweza kutumika kwa kuku wa Asili kwani kitu muhimu ni joto la kutosheleza ukuaji.

Kwa kutumia mfumo wa kubuni, kuku wanaweza kunyang'anywa vifaranga vyao mara tu baada ya kutotoa na kuviweka kwenye Bruda na hao kuku wakaachwa bila vifaranga. Baada ya majuma mawili, kuku walionyang'anywa vifaranga hao huanza tena kutaga na kuendelea na uatamiaji hadi kutotoa tena. Kwa mfumo huu kuku anaweza kutotoa mara 5 hadi 6 badala ya mara 2 hadi 3 kwa mwaka kama ilivyo sasa.


Kuna njia mbili za uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni:

**A. Njia ya uleaji wa vifaranga kwa kutumia nishati**

Utaratibu huu unahusu kutunza vifaranga kwenye mzingo (mduara) ndani ya chumba na kuvipatia joto kwa kutumia taa ya kandili (chemli), taa ya umeme au jiko la mkaa. Hata hivyo, njia hii ina gharama kubwa na wakati mwingine upatikanaji wake si wa uhakika. Kwa njia hii unaweza kupima joto katika mzingo kama linatosha au la kwa kuangalia hali ya usambaaji wa vifaranga ndani ya mzingo kama ifuatavyo:

**Mchoro namba 1: Mfano wa chombo cha kulelea vifaranga (Bruda)**

*Mchoro na. 1*




*Mduara Mwekundu Mdogo (Chanzo cha Joto)*

**Michoro namba 2 hadi namba 5, inaonyesha hali ya vifaranga inavyokuwa ndani ya chombo cha kulelea vifaranga katika hali mbalimbali za joto**


**Mchoro namba 2:** Vifaranga kusambaa ndani ya mduara wakila chakula na kunywa kwa uchangamfu, **NI DALILI KUWA JOTO LIKO SAWASAWA.**

*Mchoro na. 2*





**Mchoro namba 3:** Vifaranga kuwa pembezoni na mbali kabisa na kifaa cha joto na huku vifaranga wakipiga kelele sana, ni dalili kuwa **JOTO LIMEZIDI** na ni kali sana. Hali hii siyo nzuri kwa ustawi wa vifaranga, hivyo mfugaji anashauriwa arekebishe mara moja hali hiyo kwa kupunguza nguvu ya joto.

*Mchoro na. 3*




**Mchoro namba 4:** Vifaranga kukusanyana na kukisogelea karibu kifaa cha joto na huku wanapiga kelele sana, ni dalili kuwa **JOTO HALITOSHI.**

*Mchoro na. 4*



**Mchoro namba 5:** Vifaranga kurundikana upande mmoja inaashiria kuwa upepo ni mkali na unapuliza upande mmoja wa bruda na hivyo kuvifanya vifaranga kukimbilia upande wa pili ili kujikinga na upepo. Upepo mkali siyo mzuri kwa ustawi wa vifaranga kwani unaweza kusababisha vifo kutokana na **BARIDI KALI.**

*Mchoro na. 5*



**B. Njia ya uleaji wa vifaranga isiyotumia nishati**

Njia hii hutumika kulelea vifaranga bila ya msaada wa nishati ya kuongeza joto. Njia hii ni nzuri kwa wafugaji wadogo wadogo hasa waishio vijijini kwani hakuna gharama za kutafuta nishati ili kuwapatia joto badala yake joto la vifaranga wenyewe huwatunza na kuwapatia hifadhi maalum inayohitajika.

Zipo aina (2) za uleaji usiotumia nishati, ambazo zimebuniwa hapa nchini na kufanyiwa utafiti wa kina na kuonekana kuwa na uwezo mkubwa wa kulea vifaranga.

***1. Kutunza vifaranga kwa kutumia Kinengunengu Bruda:***

Hiki ni kifaa maalum ambacho kimebuniwa na mtaalam wa mifugo (kuku) wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Lengo la kusanifu kifaa hiki ni kuongeza kasi ya uzalishaji wa kuku wa Asili hasa vijijini. Majaribio yamefanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine Morogoro kwa vifaranga wa kisasa na wa Asili na kupata mafanikio mazuri sana.

Kinengunengu huwa kwenye umbo la mduara (mviringo) na hutumika kikiwa ndani ya chumba ili kisipigwe upepo, jua, kisilowane na mvua na kiweze kuhifadhi joto.

Kifaa hiki hutumika kulelea vifaranga bila ya msaada wa kifaa chochote cha kuwapatia joto kama kinavyohitajika kwenye mzingo, ila sehemu zenye baridi sana kifaa hiki huweza kusaidiwa na kiasi kidogo sana cha nishati kwa kutumia mkaa wa moto kidogo unaowekwa ndani ya jiko maalum na kuning'inizwa kwa juu. Jiko hili maalum litumike wakati wa mchana na liwekwe juu katikati ili kusambaza joto na Kinengunengu iwe wazi. Nyakati za jioni unaondoa jiko na kurudishia mfuniko na kufunga madirisha yote mawili.

**Jinsi Kinengunengu inavyofanya kazi:**

Huhifadhi joto la asili la vifaranga vyenyewe na kulifanya litumike tena kuwapatia joto vifaranga hao. Kwani hakuna gharama ya kutafuta nishati ili kuwapatia joto badala yake ni joto la vifaranga wenyewe ambalo huwatunza na kuwapatia hifadhi maalum inayohitajika. Kifaa hiki kinaweza kulea vifaranga 20-100. Kufutana na umbo lake, Kinengunengu huwafanya vifaranga wawe pamoja bila kutawanyika.

Vifaranga vinatakiwa vikae ndani ya Kinengunengu kwa muda wa majuma 3 hadi 4, kulingana na hali ya hewa. Baada ya hapo fungua milango ya Kinengunengu ili kuruhusu vifaranga vitoke na kuzunguka chumbani bila kuvitoa nje kwa kipindi cha mwezi mmoja au zaidi kutegemeana na mazingira. Kila inapofika jioni vifaranga virudishwe ndani ya Kinengunengu.

**Jinsi ya kutumia Kinengunengu hatua kwa hatua:**

1. Weka Kinengunengu ndani ya chumba cha kawaida kilichokuwa safi na chenye kupitisha hewa ya kutosha na wala sio chenye kupitisha upepo uvumao.
2. Weka maranda, majani makavu yaliyokatwakatwa au makapi ya mpunga chini kwa ndani ya Kinengunengu.
3. Tandika magazeti (makaratasi) juu ya maranda.
4. Weka kifaa cha maji katikati ya Kinengunengu.
5. Nyunyizia chakula cha vifaranga kiasi cha gao moja la mkono juu ya karatasi.
6. Ingiza vifaranga wako ndani ya Kinengunengu huku ukiwahesabu.
7. Fungua madirisha yote mawili ya Kinengunengu.
8. Funika mfuniko wa juu wa Kinengunengu.

**Mambo ya kuzingatia unapotumia Kinengunengu:**

- Vifaranga hukaa ndani ya Kinengunengu kwa muda wa kati ya siku saba hadi 14 bila kutolewa kutegemeana na mazingira pamoja na afya ya vifaranga vyenyewe. Joto linalotakiwa ndani ya Kinengunengu ni nyuzi joto kati ya 32 na 38. Iwapo mfugaji ana uwezo wa kununua kipima joto itamsaidia kupima na kurekebisha joto linapozidi au kupungua.
- Baada ya hapo weka uzio wa upana wa futi moja kuzunguka Kinengunengu kwa kutumia *hardboard*.
- Weka maranda ndani ya uzio uliozunguka Kinengunengu.
- Weka vyombo vya maji na chakula ndani ya uzio.
- Fungua milango yote minne iliyo chini pembezoni mwa Kinengunengu ili kuruhusu vifaranga vitoke nje kila asubuhi na kuvirudisha ndani ya Kinengunengu kila jioni hadi vifaranga vitakapofikia umri wa siku 28. Kumbuka kwamba uzio unapanuliwa kila unapoona dalili ya vifaranga kubanana.
- Baada ya siku 28 hadi 42 vifaranga wanaweza kuachiwa ndani ya chumba chote.

**Faida za kifaa hiki:**

- Kina uwezo wa kutunza vifaranga wengi kwa wakati mmoja.
- Hupunguza vifo vya vifaranga kutokana na ndege na wanyama waharibifu mfano kunguru, mwewe, vicheche, karasa.
- Kuku walionyang'anywa vifaranga vyao na kuvilea kwa msaada wa kifaa hiki, huweza kurudia kwenye mzunguko wa utagaji (wiki moja hadi wiki mbili) na kuweza kutotoa tena vifaranga kwa muda mfupi.
- Kifaa hiki hakina gharama ya nishati, na kwa zile sehemu ambazo zina baridi sana, basi huhitaji kiasi kidogo sana cha nishati

- Vifaa vinavyotumika kutengeneza kifaa hiki ni rahisi sana na hupatikana sehemu zote nchini na gharama zake ni nafuu.



*Kinengunengu Bruda inavyoonekana.*

**Vifaa vinavyotumika kutengeneza Kinengunengu:**

- *Hard board (isiyovunjika unapotengeneza mzingo).*
- Mbao 2” x 2”. Matundu hutobolewa katika mbao hizi ili kupitisha hewa safi kutoka nje kuingia ndani na hewa chafu kutoka ndani kwenda nje.
- Misumari.
- Gunia laini jepesi *(Hersian cloth).*
- Maranda au majani makavu au yaliyokaushwa (makapi ya mpunga).
- Wavu wa kuku *(chicken wire).*
- Mikono ya kushikia (sawa na mikono iwekwayo katika milango ya kabati).

**Muhimu: Kumbuka kwamba vifaranga wanapopiga kelele sana (kulia) ndani ya Bruda yoyote ile inaashiria, joto limezidi au kupungua mno, kutokuwepo maji au chakula au usumbufu (inaweza kuwa wadudu, unyevunyevu unaosababishwa na maji kumwagika au upungufu wa hewa).**

### 2. *Kutunza vifaranga kwa kutumia Mkombozi Bruda*

Mkombozi Bruda ni kifaa maalum ambacho kimebuniwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na kufanyiwa majaribio huko Mlandizi, Pwani kwa kuku wa Asili na kimeonyesha mafanikio mazuri. Kifaa hiki kimeitwa Mkombozi kwa kuwa ni rahisi kukitengeneza na hata kukitumia na pia kimeonyesha mafanikio katika kulea vifaranga.

**Namna Mkombozi Bruda inavyofanya kazi**

Huhifadhi joto la asili la vifaranga vyenyewe na kulifanya litumike tena kuwapatia joto vifaranga hao. Kwani hakuna gharama ya kutafuta nishati ili kuwapatia joto badala yake ni joto la vifaranga wenyewe ambalo huwatunza na kuwapatia hifadhi maalum inayohitajika. Kifaa hiki kinaweza kulea vifaranga 20 mpaka 70.

Vifaranga hulelewa kwa wiki 8 na baada ya hapo huhamishiwa katika banda la kuku wanaokua. Wakati wa usiku, vifaranga hufungiwa kwenye sehemu ya kuhifadhi joto na hutenganishwa na sehemu ya kuzungukia. Chakula na maji safi huwekwa kwenye sehemu ya kuzungukia wakati wote wa mchana.

Wiki ya kwanza vifaranga hutolewa kwenye sehemu ya kuhifadhi joto (wanapolala vifaranga) na kuwekwa sehemu ya kuzungukia (wanaposhinda vifaranga) kwa ajili ya kupewa chakula na maji.

Baada ya wiki ya kwanza milango ya vifaranga ifunguliwe wakati wa mchana na vifaranga waruhusiwe kuzunguka sehemu ya kushindia. Mkombozi ihamishwe mara kwa mara kuruhusu vifaranga kupata majani mabichi, wadudu na rasimali nyingine za vyakula.



*Mkombozi Bruda inavvyoonekana.*

Wiki ya kwanza Mkombozi huweza kuhifadhi nyuzi joto kati ya 34C na 39C. Hata hivyo kiwango cha joto hupunguzwa kwa nyuzi joto 3C kila wiki kwa kupunguza majani makavu katikati ya kiota na kuta za Mkombozi kwenye mfuniko. Nafasi katika kiota huongezwa kila wiki kwa kupunguza maranda ya mbao katika Mkombozi . Mkombozi huwa na mzunguko wa hewa safi na ya kutosha kwa kutoboa vishimo vidogo 16 ikiwa ni matundu 4 kwa kila upande wa pembeni mwa Bruda au kujenga sakafu kwa kutumia wavu.

**Namna ya kutengeneza Mkombozi Bruda:**

Muundo wa Mkombozi umejumuisha sehemu ya kuhifadhi joto na sehemu ambayo huruhusu vifaranga kuzunguka.

Sehemu ya kuhifadhi joto na ambapo vifaranga hulala hutengenezwa kwa vipande vinne vya mbao. Vipande hivyo, vina upana wa sentimita 30 na unene wa sentimita 3. Upana na urefu wa sehemu ya kuhifadhi joto hutegemea idadi ya vifaranga wanaotarajiwa kulelewa. Hali kadhalika, sehemu ya kuzunguka hutengenezwa kwa vipande vinne vya mbao, vipande hivyo vina upana wa sentimita 30 na unene wa sentimita 3. Upana na urefu wa sehemu ya kuzungukia hutegemea idadi ya vifaranga wanaotarajiwa kulelewa.

**Jedwali namba 5: Vipimo vya utengenezaji wa Mkombozi Bruda**

| Idadi ya Vifaranga | Vipimo sehemu ya kuhifadhi Joto (sm) (Wanapolala vifaranga) | | | Vipimo sehemu ya Kuzungukia (sm) (Wanaposhinda vifaranga) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kina | Urefu | Upana | Kina | Urefu | Upana |
| 20 | 30 | 26 | 26 | 30 | 56 | 56 |
| 30 | 30 | 37 | 37 | 30 | 80 | 80 |
| 40 | 30 | 45 | 45 | 30 | 98 | 98 |
| 50 | 30 | 52 | 52 | 30 | 113 | 113 |
| 60 | 30 | 63 | 63 | 30 | 139 | 139 |
| 70 | 30 | 68 | 68 | 30 | 150 | 150 |

*Kutengeneza sehemu ya kuhifadhi joto:*

Unganisha vipande hivyo vya mbao ili kupata umbo la mraba. Toboa matundu 4 kila upande wa juu wa umbo la mraba (unaweza kutoboa kwa kutumia Keikei au kifaa chochote kinachoweza kutoboa tundu). Kwahiyo, jumla ya matundu yatakuwa 16. Toboa mlango upande mmoja ambao vipimo vyake vitategemea ukubwa wa Mkombozi Bruda. Tengeneza sehemu ya sakafu kwa kutumia mbao nyepesi ili kupunguza gharama. Pia unaweza kutumia wavu (Coffee Wire) ili kuruhusu hewa ya kutosha kwenye Bruda. Kama utatumia wavu, inashauriwa ufunike na karatasi haswa wakati wa msimu wa mvua. Unaweza kutengeneza sehemu ya kiota kwa wavu au kwa karatasi ngumu (Hard

Board). Unapotumia wavu, zungusha sehemu ya ndani ya kiota na kuacha sehemu ya mlango tu. Pia fanya hivyo hivyo unapotumia karatasi ngumu (Hard Board). Weka majani makavu au maranda baina ya kuta za mbao na wavu bila kushindilia. Paa au mfuniko huzungushwa kwa gunia lenye mkunjo mmoja au miwili na kuweka majani makavu au maranda kwa madhumuni ya kuhifadhi joto. Juu ya sehemu ya kuzungukia ambamo vifaranga hushinda huweza kufunikwa na wavu au vifaa vingine vyovyote vilivyo rahisi kupatikana, kama vile fito za mianzi au miti ili mradi viweze kuwalinda vifaranga dhidi ya maadui.

**Mafunzo yafuatayo yanapaswa kufanywa kwa vitendo:**

- **Ushikaji wa kuku unaofaa.**
- **Uandaaji wa sehemu ya kulelea vifaranga.**

## Mada ya 9: Tabia Chache Mbaya Zinazoweza Kujitokeza Miongoni mwa Kuku wa Asili

Tabia mbaya au kwa kiingereza '*vices*' miongoni mwa kuku wa Asili mara nyingi siyo jambo linalotokea mara kwa mara. Hata hivyo, kuna baadhi ya tabia mbaya ambazo kuku wa Asili anaweza kuwa nazo. Tabia hizi ni pamoja na ulaji wa mayai na kudonoana. Tatizo kubwa kati ya haya matatizo mawili ni ulaji wa mayai.

**Jedwali na 5: Muhtasari wa mambo yanayoweza kusababababisha tabia mbaya za kuku na hatua za kuchukuwa ili kuzuia hali hiyo**

| Na. | Tabia | Sababu | Kuzuia/Kinga |
|---|---|---|---|
| 1. | Ulaji wa Mayai | Tabia ya kurithi kutoka vizazi vya nyuma | Ondoa kutoka katika kundi kuku wenye kuonyesha muelekeo huo |
| | | Kukosekana au kuwa na viota vichache sehemu za kutagia | Weka viota vya kutosha, angalau viwe nusu ya idadi ya kuku wanaotaga |
| | | Msongamano wa kuku | Weka/fuga idadi ya kuku kulingana na nafasi au eneo lililopo |
| | | Kuku kuwa na sehemu moja tu kwa kulala na kutaga | Tenganisha sehemu ya kulala na kutagia |
| | | Viota vya kutagia kuwekwa sehemu isiyo ya faragha na mwanga mkali | Viota viwekwe sehemu ya faragha na yenye kiza kidogo |
| | | Chakula chenye ukosefu/upungufu wa protini na madini ya chokaa | Kuku wapewe chakula chenye mchanganyiko sahihi wa viini lishe vya protini na madini ya chokaa |
| | | Kubadilika kwa hali ya hewa kwenye banda, mfano joto kali, unyevunyevu na ukavu sana (vumbi). | Weka banda la kuku katika hali ya usafi |
| 2. | Kudonoana | Kuku kuwekwa kwenye msongamano na haswa kwa ufugaji wa ndani | Fuga kuku wa asili kwa mtindo wa nusu huria au nusu nje nusu ndani<br>Kukata midomo ya kuku kulingana na ushauri wa mtaalam |

**Mafunzo yafuatayo yanapaswa kufanywa kwa vitendo:**

- **Kutambua tabia zisizofaa kwenye kuku na ukataji wa midomo ya kuku.**

## A. Magonjwa yashambuliayo kuku wa asili:

Changamoto na kikwazo kikubwa cha kuku wa Asili ni magonjwa yanayoshambulia kuku mara kwa mara. Kwa kuwa magonjwa mengi hatari ya kuku hayana tiba, inatakiwa kinga kufuatiliwa na kutolewa katika muda muafaka. Mada hii itaelezea kwa ufupi aina ya magonjwa jinsi yanavyoambukizwa, dalili, kinga na tiba.

**Baadhi ya magonjwa hatari yashambuliayo kuku wa Asili:**

- Kideri/Mdondo *(New Castle Disease)*
- Ndui ya kuku *(Fowl pox)*
- *Kipindupindu cha Kuku (Fowl Cholera)*
- Mafua ya kuku *(Infectious Coryza)*
- Homa ya matumbo *(Fowl Typhoid)*
- Kuhara damu *(Coccidiosis)*
- Ukosefu wa Vitamini A
- Minyoo na wadudu kama viroboto, chawa, utitiri na kupe wa kuku.

### 1. Kideri/Mdondo *(New Castle Disease)*

Ugonjwa huu huwapata kuku wakubwa na wadogo na ni miongoni mwa magonjwa hatari ambayo huambukizwa kwa kasi kubwa sana na kusababisha vifo. Ugonjwa huu husababishwa na virusi na huweza kushambulia pia bata, bata mzinga, kanga, kwale na ndege wengineo.

**Jinsi unavyoambukiza:**

- Kuku mzima kuvuta hewa yenye virusi vya ugonjwa huu toka kwa kuku mgonjwa.
- Upepo huweza kuhamisha virusi vya ugonjwa huu toka sehemu hadi sehemu.
- Watu huweza kuhamisha ugonjwa huu wanapotembea toka sehemu hadi sehemu.
- Kuku wasio na ugonjwa wakikaa pamoja na kuku wagonjwa.
- Ndege wanaokula mizoga kama kunguru huweza kusambaza mabaki ya mizoga yenye ugonjwa huu.
- Vyombo vya usafiri toka kwenye eneo lenye ugonjwa.

**Dalili zake:**

- Homa kali, kuku kuwa dhaifu, kuzubaa na kushusha mabawa na kupoteza hamu ya kula.
- Kuku kupoteza fahamu na kupooza viungo.
- Kulegea kwa shingo na inaweza kupinda kuelekea nyuma au pembeni pia huweza kuzungusha shingo.
- Kuhema kwa shida na hutoa majimaji mdomoni yenye harufu kali.

- Kukohoa, kukoroma  na kupiga chafya.
- Kuharisha kinyesi chenye rangi ya kijani.
- Vifo vya mfululizo vinavyoweza kumaliza kuku wote bandani.

**Matibabu ya Kideri: Ugonjwa huu unaambukizwa na virusi, hivyo basi hauna tiba, bali kinga.**

**Kinga ya ugonjwa:**

- Kuku wasio na ugonjwa wapatiwe chanjo mapema.
- Vifaranga wapatiwe chanjo wakiwa na siku tatu (3).
- Chanjo irudiwe kila baada ya miezi mitatu
- Kuku wagonjwa wauawe na mizoga yao ichomwe moto na kufukiwa.
- Hakikisha usafi wa banda la kuku na vyombo vyote wanavyotumia.

**Muhimu: Usichanje kuku kama ugonjwa umeshaingia kwenye kundi.**

**Kuna aina mbili za chanjo ya mdondo:**

***1. Chanjo inayoweza kuvumilia joto (Thermostable):***

Chanjo hii inaweza kutunzwa katika hali ya joto la kawaida *(room temperature)* na kuendelea kubaki salama kwa muda wa siku 30. Hutolewa kwa kuku kwa njia ya matone kwenye macho. Kwa kutumia chanjo hii unaweza kuwachanja kuku muda wowote katika siku. Ila inashauriwa kuwa chanja asubuhi ili kupunguza uwezekano wa chanjo kupata miale ya jua ya moja kwa moja.



*Kuku wakipewa chanjo ya mdondo*

**Muhimu: Inashauriwa kuweka chanjo hii chini ya chombo kinachoweka mtungi wa maji kama hauna friji. Hii huongeza zaidi usalama wa chanjo hiyo. Usiweke chanjo kwenye paa kwani joto laweza kuwa kali zaidi. Pia si vyema kubeba chanjo kwenye karatasi za plastiki kwani hizi huweza kuongeza joto zaidi.**

***2. Chanjo isiyovumilia joto:***

Chanjo hii hutunzwa kwenye ubaridi muda wote. Hutolewa kwa kuku kwa kuchanganywa na maji ya kunywa kuku. Ikishachanganywa, huchukua muda mfupi kama wa saa moja na baada ya hapo inaanza kupoteza ubora wake. Kwa hali hiyo, inashauriwa kuwanyima kuku maji kwa muda ili wapate kiu sana na ndipo uwawekee maji ya kunywa yenye chanjo ili wayanywe kwa wingi na kwa muda mfupi. Pia inashauriwa kuwa siku ya chanjo wape kuku chakula kikavu zaidi kabla ili wapate kiu sana.

**Muhimu:**

- Mdondo au kideri ni ugonjwa tishio ambao huweza kuua kuku wote.
- Mdondo ukitokea vifo huwa vingi, kuku hupumua kwa taabu, hupooza na wengine huzunguka na kuzungusha kichwa.
- Mdondo huweza kuzuiwa kwa chanjo kila baada ya miezi mitatu.
- Wafugaji kuku waunde vikundi vya ushirika wa kuchanja mdondo.

**2. Ndui ya kuku *(Fowl Pox)*:**

Ugonjwa huu huwashambulia kuku wadogo na wakubwa, na husababishwa na virusi.

**Jinsi unavyoambukiza:**

- Ugonjwa huu huambukizwa kwa kupitia kwenye vijeraha vya kuku.
- Mbu na wadudu wengine waumao huweza kuambukiza anapomuuma kuku mgonjwa na halafu akamuuma kuku asiye na ugonjwa.



*Kuku mwenye ndui*

**Dalili zake:**

- Homa kali.
- Kupoteza hamu ya kula.
- Kupoteza uzito.
- Kutokea kwa vipele sehemu mbalimbali zisizo na manyoya.
- Baada ya siku kati ya 7 hadi 14 vipele hupasuka na kuacha vidonda.
- Vifo huweza kutokea kwa kuku wenye umri mdogo.
- Kutoa kamasi kwenye pua.
- Mara nyingi vipele husababisha kuziba macho.

**Matibabu:** Ugonjwa huu hauna tiba, kwani huambukizwa na virusi. Ila inashauriwa kuwapa kuku dawa ya *antibiotic* ili kuzuia kutibu magonjwa nyemelezi yanayoweza kuwashambulia kuku kupitia kwenye vidonda.

**Kinga:**

- Ndui ya kuku huzuiwa kwa chanjo ya sindano.
- Vifaranga wapatiwe chanjo wakiwa na umri wa siku moja na kurudiwa baada ya miezi 2 hadi 3.
- Tenga kuku wagonjwa na wazima.
- Epuka madimbwi karibu na nyumbani ili kuepusha mazalia ya mbu.

**Muhimu: Ili kupunguza kasi endapo ugonjwa huu umewapata kuku, sugua majeraha au vipele kwa pamba iliyochovywa kwenye dawa ya madini joto *(Iodine)* na baadaye paka mafuta mazito *(Petroleum jelly)* au samli. Hii si kutibu ugonjwa bali unawasaidia kuku kulainisha ngozi na macho yapate kuona chakula na maji.**

### 3. Homa ya Matumbo *(Fowl Typhoid)*:

Ugonjwa huu husababishwa na Bakteria na huwapata kuku wa umri wote. Ugonjwa huu huambukizwa kutoka kwa kuku wagonjwa kwenda kwa kuku wasio wagonjwa, kupitia kwenye mayai, chakula chenye kinyesi cha kuku wenye ugonjwa pia watu iwapo watabeba vimelea na kuja navyo kwenye banda.

**Jinsi unavyoambukiza:**

- Kuku asiye mgonjwa kula vimelea vya ugonjwa kupitia kinyesi cha kuku mgonjwa kwenye chakula.
- Kuku mgonjwa huweza kurithisha vifaranga wake kupitia mayai aliyotaga.
- Watu na vyombo vya usafiri wanaweza kuhamisha ugonjwa kutoka sehemu hadi sehemu.

- Vyakula vya kuku kutoka sehemu yenye ugonjwa kwenda kusiko na ugonjwa.
- Mizoga ya kuku yenye ugonjwa ikipelekwa sehemu isiyo na ugonjwa.

**Dalili:**

- Homa kali.
- Manyoya husimama.
- Kinyesi kuonekana kuganda sehemu ya nyuma.
- Kukosa hamu ya kula.
- Kuku kudhoofika.
- Kiwango cha utagaji hushuka.

**Kinga:**

- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa.
- Kuku wagonjwa watengwe na kupewa tiba ya *antibiotic*.
- Zingatia usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji.

**Matibabu:**

Dawa aina ya *Oxytetracycline (OTC)* au Salfa ambayo huchanganywa kwenye maji na kupewa kuku kwa siku 5 hadi 7.

**4. Mafua ya kuku *(Infectious Coryza)*:**

Ugonjwa huu husababishwa na bakteria na hushambulia sana hasa kuku wakubwa. Bakteria hawa hupenda kuishi kwenye mavumbi.

**Jinsi unavyoambukiza:**

- Kuku asiye mgonjwa kula chakula au kuvuta hewa yenye vimelea vya ugonjwa huu.
- Kuku wazima wanapochanganywa na wagonjwa.

**Dalili:**

- Kuvimba uso chini na nyuma ya jicho.
- Kupumua kwa matatizo na hata kukoroma.
- Kuvimba kwa macho.
- Kushindwa kula.
- Kutoka makamasi puani.
- Kutoa usaha unaonuka.

- Kuchafuka mbawa.

**Matibabu:** Dawa za Salfa au *Antibiotic*.

**5. Kuhara damu *(Coccidiosis)*:**

Ugonjwa huu husababishwa na vimelea aina ya *Protozoa* na hushambulia kuku wote wakubwa na wadogo ila huathiri zaidi kuku wadogo.

**Jinsi unavyoambukiza:**

- Kula chakula chenye kinyesi au maji yenye vimelea vya ugonjwa huu.

**Dalili:**

- Kuharisha kinyesi kilichochanganyika na damu.
- Kuku kudhoofu na kupungua uzito.
- Kuku kuzubaa na kushusha mabawa kama kavaa koti.
- Kuku kujitenga na wengine.
- Kupoteza hamu ya kula.



*Vifaranga wakiwa na ugonjwa wa kuhara damu.*

**Tiba:**

Dawa aina ya *Amprolium, Oxytetracycline* au Salfa ambayo huchanganywa kwenye maji na kupewa kuku kwa siku 5 hadi 7.

**Kinga:**

- Vifaranga wakifikia umri wa siku saba (7) wapewe *Amprolium* kwa siku tatu (3) mfululizo, hata kama dalili za ugonjwa hazijajitokeza.
- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa
- Kuku wagonjwa watengwe na kupewa tiba mara moja
- Zingatia usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji

**6. Kipindupindu cha Kuku *(Fowl Cholera)*:**

Kipindupindu cha kuku husababishwa na bakteria.

**Dalili:**

- Kuharisha kinyesi cha njano.
- Kusinzia na kulegea.
- Kuhema kwa shida.
- Kushindwa kusimama.
- Kulala huku kichwa kimening'inizwa kwenye mabawa.
- Kuwa na uvimbe kwenye mikunjo ya miguu.
- Kutoa kamasi puani.

**Tiba:**

- Dawa aina ya *Oxytetracycline (OTC)* au Salfa ambayo huchanganywa kwenye maji na kupewa kuku kwa siku 5 hadi 7.

**Kinga:**

- Chanja kuku wakiwa na umri wa miezi mitatu (3).
- Zingatia usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji.

**Ukosefu wa Vitamini 'A':**

Ukosefu wa vitamini 'A' ni tatizo la lishe ambalo huwakabili kuku kutokana na ukosefu wa chakula chenye vitamini hii. Mara kwa mara hujitokeza baada ya kipindi kirefu cha kiangazi kwa ajili ya ukosefu wa majani mabichi.

**Dalili za ukosefu wa vitamini 'A':**

- Kuku kudumaa kutokana na kutokula vizuri.
- Macho huvimba na kutoa uchafu mzito kama sabuni iliyolowana.



*Dalili za kuku mwenye upungufu wa Vitamini A.*

**Tiba:**

- Hakuna tiba itakayomponyesha kuku baada ya dalili hizi kujitokeza na matokeo yake ni kifo.
- Hata hivyo kuku wote waliobakia katika banda lako wapewe dawa ya vitamini za kuku ambazo pia huwa na vitamini A kwani watakuwa na upungufu japokuwa dalili za ugonjwa hazijajitokeza.

**Kinga:**

Hakikisha kuku wanapata majani ya kijani katika malisho yao. Walimie mchicha au wachumie majani mabichi kutoka sehemu zenye maji. Unaweza kuwapa vitamini za kuku za dukani kwa kufuata mapendekezo  ya watengenezaji.

**B. Wadudu washambuliao kuku wa Asili:**

Kuku hushambuliwa na wadudu wa aina mbalimbali ambao wamegawanyika katika makundi makuu mawili kama ifuatavyo:

1. Wadudu wanaoshambulia ndani ya mwili.
2. Wadudu wanaoshambulia nje ya mwili (juu ya ngozi).

Wadudu hawa humnyonya kuku damu na kumfanya adhoofike, kupata magonjwa kwa urahisi na hatimaye kifo.

**1. Wadudu washambuliao ndani ya mwili:**

***a) Minyoo:***

Kuna minyoo ya aina nyingi inayoshambulia kuku na kusababisha kupungua kwa utagaji na udhoofu wa kuku. Katika minyoo yote, minyoo ya mviringo *(Ascaris)* hushambulia sana kuku na kusababisha madhara makubwa.

**Dalili za minyoo:**

- Upungufu wa hamu ya kula.
- Kudumaa kwa kuku wanaokua.
- Kupungua kwa utagaji.
- Minyoo mingine husababisha kupumua kwa shida.
- Kuku hupungua uzito.
- Minyoo kuonekana kwenye kinyesi.

**Kutibu na kuzuia minyoo:**

Minyoo mingi huuliwa na dawa ya *Piperazine* hivyo basi ni muhimu kuku kupewa dawa ya minyoo

kila baada ya miezi mitatu. Fanya usafi wa mabanda na kuhakikisha kwamba mabanda ya kuku hayana unyevunyevu.

**2. Vidusia wa nje washambuliao kuku:**

Hawa ni wadudu wanaokaa kwenye manyoya na ngozi. Wadudu hawa ni pamoja na Viroboto, Papasi, Chawa, Utitiri na wengineo. Wadudu hawa huwasumbua sana kuku na kuwafanya kutumia muda mwingi kujikuna na kujigaragaza kwenye vumbi badala ya kula.

***a) Viroboto, Chawa, Utitiri, Kupe, Papasi***

- Viroboto ni tatizo kubwa kwa vifaranga, hunyonya damu hadi kuua.
- Utitiri hunyonya damu na huathiri sana kuku wanaoatamia.

**Chanzo cha kuwepo wadudu:**

- Mipasuko sakafuni na kwenye kuta.
- Uchafu uliokithiri wa mazingira.
- Kuingiza kuku wageni kwenye kundi bila kuchukua tahadhari.

**Njia za Kuzuia Vidusia wa Nje:**

- Zingatia usafi wa banda la kuku.
- Nyunyiza majivu au chokaa au dawa za kuua wadudu kila mara unapofanya usafi wa banda.
- Choma masalia ya mayai yaliyoanguliwa.
- Tumia dawa ya unga ya kuua wadudu kwa kuwanyunyizia kuku, kwenye viota vya kutagia na sehemu zote za banda.
- Badilisha matandiko kila unapoona yanatakiwa kubadilishwa na uyapeleke shambani.

**Dalili:**

- Kufubaa kwa manyoya.
- Rangi ya upanga kuwa hafifu kutokana na upungufu wa damu.
- Kukosa hamu ya chakula.
- Ngozi kuwa nene, ngumu na yenye magamba yanayodondoka kama unga mweupe.
- Kupungua uzito.
- Kujikunakuna kwa kuku.
- Wadudu kuonekana kwa macho.

**Athari za wadudu washambuliao kuku:**

- Kuku anayeatamia hatulii kwenye kiota, hii husababisha kutotoa vifaranga wachache.

- Kupungua au kukoma kwa utagaji.
- Ukuaji wa taratibu.
- Ulaji hafifu.



*Kifaranga kilichoshambuliwa na viroboto.*

**Muhimu:**

Magonjwa ni chanzo kikuu cha vifo kwa kuku wa Asili na hii husababisha hasara katika ufugaji, hivyo basi:

- Kinga ni bora kuliko tiba.
- Fanya usafi wa mabanda yako ya kuku mara kwa mara.
- Hakikisha vyombo vya chakula na maji ni visafi.
- Toa lishe iliyokamilika na ya kutosha.
- Pata ushauri wa mara kwa mara kutoka kwa wataalamu wa mifugo waliopo karibu na makazi yako.
- Kuku wageni watengwe kwa muda usiopungua siku 14 kabla hawajachanganywa na kuku wenyeji na wapewe chanjo.

**Mafunzo yafuatayo yanapaswa kufanywa kwa vitendo:**

- **Uchanjaji wa kuku ili kuzuia maradhi.**
- **Kutoa dawa ya utitiri, viroboto na chawa.**
- **Kutoa dawa ya minyoo.**
- **Kusafisha mabanda ya kuku kwa kutumia dawa.**

Madawa ya asili yatokanayo na mimea yanayosaidia katika tiba na kinga za maradhi mbalimbali ya kuku.

**A. Sehemu za mimea zinaweza kuwa: Majani, Magome, Mbegu, Maua au Matunda**

**B. Umuhimu wa kutumia tiba zenye asili ya mimea:**

- Hupatikana kwa urahisi.
- Ni rahisi kutumia.
- Gharama nafuu.
- Zinatibu vizuri.
- Hazina madhara.

**C. Baadhi ya mimea inayotibu maradhi ya kuku:**

**1. Mwarobaini** (Majani, Mizizi, Magome): Hutibu magonjwa yafuatayo:

- Typhoid.
- Kuzuia Kideri.
- Kuhara.
- Mafua.
- Vidonda.

**2. Shubiri Mwitu** *(Aloe vera):*

Chukua majani 3-5 makubwa, katakata na loweka ndani ya maji lita 10 kwa masaa 12 hadi 16. Wape kuku kwa siku 5 - 7. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine baada ya masaa 12. Mchanganyiko huu unaweza kutibu:

- Kideri/Mdondo (Mdonde/Chikwemba/Kitoga/Chinoya/Sotoka) - inyweshwe kabla kwa kinga.
- Homa ya matumbo *(Typhoid).*
- Mafua *(Coryza).*
- Kipindupindu cha kuku *(Fowl Cholera).*



*Shubiri Mwitu*



Mtakalang’onyo

**3. Mtakalang’onyo** *(Euphorbia):*

Majani makubwa 3-5, ponda, weka katika lita 10 za maji kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine. Mtakalang’onyo hutibu:

- Kideri/Mdondo (Mdonde/Chikwemba) - inyweshwe kabla kuzuia
- Gumboro.
- Ndui.
- Kuhara damu *(Coccidiosis)*.

**4. Mbarika (Nyonyo):**

Hutibu Uvimbe. Weka majani ya mbarika ndani ya majani ya mgomba kisha weka ndani ya jivu la moto, kisha kanda sehemu yenye uvimbe kwa kutumia majani hayo ya mbarika.

**5. Mlonge** *(Mlonje):*

Ina vitamini A na C. Chukua majani ujazo wa mikono miwili (gao mbili). Kisha yapondeponde na kuyaweka katika lita 10 za maji na iache kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine. Mlonge hutibu:

- Mafua.
- Kideri - inyweshwe kabla kwa kukinga
- Kipindupindu cha kuku *(Fowl Cholera).*
- Homa ya matumbo
- Ini.

**6. Konfrei:**

- Ina madini na vitamini nyingi.
- Hutibu vidonda na majipu.

**7. Ndulele** *(Dungurusi, Makonde, Tura/Ndula):*

- Majani hutibu Minyoo.
- Matunda hutibu Vidonda.

**8. Papai** *(Majani):*

Chemsha magao mawili ndani ya maji lita 6 hadi ubakie na lita 1. Poza kisha chuja. Hutibu:

- Minyoo

**9. Mwembe:**

Majani magao mawili, ponda na chemsha ndani ya lita 6 za maji hadi ibaki lita 1. Wape kwa siku moja. Mwembe hutibu:

- Homa ya matumbo.
- Mafua.
- Kinga ya Kideri/Mdondo.

**10. Mpira:**

Chemsha majani au mizizi. Mpira hutibu:

- Tumbo
- Vidonda na majipu

**11. Minyaa** *(Cactus):*

Hii ni aina yenye majani manene-hadi kufikia nusu nchi na mapana hadi kufikia upana wa viganja viwili vya mikono. Minyaa hutibu: (Angalia inaunguza au kubabua).

- Vidonda.
- Ngozi.
- Uzazi.



*Minyaa (Cactus)*

**12. Pilipili Kichaa:**

Pondaponda kiasi kisha changanya na maji na wawekee kuku wawe wanakunywa kwa muda wao. Inasemekana inasaidia kutibu mdonde (lakini mapema kabla maradhi kuingia).

Kumbukumbu za mradi wa kuku ni muhimu sana katika mazingira ya sasa ambayo kuku hufugwa kwa ajili ya biashara zaidi na sio kitoweo tu. Kumbukumbu hizi endapo zitatunzwa vizuri zitamwezesha mfugaji kusimamia mradi wake vizuri na kutambua kama shughuli zake za ufugaji zinafanyika kwa ufanisi mkubwa au la. Pia kumbukumbu hizi zitasaidia kuonyesha yafutayo:

a. Faida au hasara inayotokana na kuendesha shughuli za ufugaji.
b. Mtindo na namna ya utendaji wa shughuli za ufugaji.
c. Matukio muhimu yaliyotokea ndani ya mradi kama vile aina ya magonjw yaliyoshambulia kuku na chanjo na tiba zilizotumika, kiwango cha utagaji wa mayai n.k.
d. Kuonyesha kwa undani namna ya shughuli ilivyoendeshwa muda uliopita au mbinu zilizotumika.
e. Maendeleo ya kuku.
f. Aina ya Magonjwa yaliyoshambulia kuku.
g. Chanjo na tiba zilizofanyika.

**1. Faida za kumbukumbu:**

a. Zinamuwezesha kugundua makosa na kuweka mpangilio wa masahihisho ya makosa
b. Ni namna ya kuongeza na kuendeleza uwezo wa usimamizi na uongozi wa mfugaji.
c. Huwezesha kufanya maamuzi sahihi yahusuyo mradi.

**Matatizo yanayojitokeza katika uwekaji wa kumbukumbu:**

a. Ukosefu wa ujuzi na elimu ya jinsi ya kuweka kumbukumbu.
b. Uwekaji wa baadhi ya kumbukumbu ambazo haziwezi kusaidia kubadilisha mwenendo wa mradi husika.

**2. Kumbukumbu zimegawanyika katika sehemu zifuatazo:**

a. Kumbukumbu za uzalishaji.
b. Kumbukumbu za fedha.
c. Kumbukumbu za rasilimali zote katika uzalishaji.
d. Kumbukumbu za matibabu na kinga.

***a. Kumbukumbu za uzalishaji:***

Hizi zitamwezesha mfugaji kujua kiasi cha mayai yanayotagwa na vifaranga waliototolewa pia kujua idadi ya kuku wanaokufa kwenye banda lake hivyo aweze kuchukua tahadhari.

***b. Kumbukumbu za fedha, matumizi na mapato:***

Hizi zitamsaidia mfugaji kujua uwiano wa mapato na matumizi ili aweze kujua kama anapata faida au hasara ya mradi wa ufugaji wa kuku.

**Mfano wa kumbukumbu:**

**a. Idadi ya Kuku:**

| Mwezi | | | | | Mwaka | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | Idadi ya Kuku | | | | Vifo/Mauzo | Baki | Maelezo |
| | Mitetea | Majogoo | Vifaranga | Jumla | | | |
| 1 | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | |

**b. Kumbukumbu ya Uatamiaji na Utotoaji:**

| Tarehe/Mwezi | Idadi ya Mayai | | | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | Yaliyoatamiwa | Yaliyoanguliwa | Yasiyoaanguliwa | |
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| **Jumla** | | | | |

**c. Kalenda ya Chanjo/Tiba:**


| Ugonjwa | Miezi | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| **Mdondo** | | | | | | | | | | | | |
| **Ndui** | | | | | | | | | | | | |
| **Gumboro** | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | |

**d. Mapato na Matumizi:**

| Matumizi | | | Mapato | |
|---|---|---|---|---|
| Tarehe/Mwezi | Shughuli | Kiasi cha Fedha | Chanzo | Kiasi cha Fedha |
| **1** | | | | |
| **2** | | | | |
| **3** | | | | |
| **4** | | | | |
| **Jumla** | | | | |

**Mafunzo yafuatayo yanapaswa kufanywa kwa vitendo:**

- **Uwekaji wa kumbukumbu.**



*Mfugaji akifurahia zao la mayai kutoka kwenye mradi wake wa kuku na wakati huohuo kuandika vitabu vyake vya kumbukumbu.*

# Mada ya 13: Ujasiriamali

**Utangulizi**
Ujasiriamali ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Nchi. Wajasiriamali hushiriki haswa kwenye kuanzisha na kusimamia shughuli zao za kibiashara kwa ujasiri kwa lengo la kupata faida.  Kufanya hivyo huleta matokeo ya matumizi bora ya mali zilizopo, utoaji wa rasilimali kwa mashirika mengine na uzalishaji wa ajira.

Ujasiriamali ni pamoja na kutambua fursa na jinsi ya kuanzisha biashara, utafutaji wa masoko na kuweka mipango ya uwekezaji.

**Maana ya Ujasiriamali**
Ujasiriamali ni uwezo wa kukubali kuingia katika biashara, kumiliki na kusimamia jambo kwa ujasiri. Ujasiriamali unahusu utafutaji, ushawishi na uendeshaji wa shughuli yako kibiashara kwa lengo la kupata faida.

***Jedwali na. 13:*** **Sifa, Mtazamo na Matendo ya Mjasiriamali**

| Sifa | Mtazamo na Matendo yake |
|---|---|
| Anayo nia na ari ya jambo aliloamua kulifanya | • Ana uwezo wa kutoa uamuzi mapema hata kama ni mgumu.<br>• Yuko tayari na hujitolea yeye binafsi.<br>• Hufanya kazi yake kwa nidhamu ya juu.<br>• Hakati tamaa.<br>• Ana uwezo wa kutatua matatizo |
| Hupenda kutumia fursa inayojitokeza kikamilifu. | • Anatambua mahitaji ya wateja wake kwa uhakika.<br>• Anajua na kufuata mwelekeo wa soko<br>• Anapenda kufanya kitu ambacho kinaonekana mbele ya jamii.<br>• Hafanyi mambo kwa pupa. |
| Anao uwezo na kipaji cha kuwasiliana, kuongoza pia kushawishi na daima mbele kwa kila analotenda. | • Anapenda kushirikiana<br>• Anapenda kuwahamasisha wengine<br>• Anaheshimika na anaaminika.<br>• Mpenda haki<br>• Hupenda kujifunza na kufundisha wengine.<br>• Hukubali wengine kumkosoa<br>• Hana ubinafsi. |
| Mvumilivu, yupo tayari kuchukua uamuzi ambao unaweza kuhatarisha biashara yake na kwake binafsi. | • Mpenda kujitosa – liwalo liwe.<br>• Hushirikisha wengine katika matatizo ya biashara.<br>• Ana uwezo wa kufanya biashara kwenye mazingira yaliyoeleweka.<br>• Huvumilia hata penye mambo ambayo hana uhakika kama yatafanikiwa.<br>• Hujitia moyo hata kama mambo yakienda vibaya.<br>• Anayo nia na ari ya kutenda. |
| Ana ari na msukumo mkubwa wa kufanikiwa katika shughuli zake. | • Anajua uwezo na mapungufu yake.<br>• Anapenda ushindaji wa maendeleo<br>• Anaweka malengo ya juu lakini anayoweza kutekeleza.<br>• Anapenda kuweka malengo na kufanya kila liwezekanalo ili kufanikisha azma yake.<br>• Hapendi kulaumu pale anaposhindwa kutimiza malengo yake.<br>• Hapendi malumbano, bali hutafuta mbinu za kupambana na vikwazo.<br>• Ni mpenda watu na daima mwenye furaha. |
| Mtundu, Mbunifu na Mpenda kujitegemea | • Ni mbunifu katika kupambana na kutatua matatizo.<br>• Ana uwezo wa kujifunza kitu kwa haraka.<br>• Haogopi kushindwa.<br>• Ana uwezo wa kuzoa mawazo pia mambo mapya kwa haraka<br>• Ana uwezo wa uchambuzi wa hakika kwa manufaa ya biashara yake.<br>• Mpenda mabadiliko. |
| Kujiwekea malengo ya muda mfupi na mrefu. | • Hupenda kufanya kazi zake kwa mpangilio maalumu.<br>• Hutazama mbele. |

**Kanuni za Mfanya biashara, Mtafutaji/Mjasiriamali**

- Huangalia ukweli wa mambo kwa kujifunza kadri iwezekanavyo kuhusu biashara yake.
- Huangalia na hufahamu sehemu imara za biashara yake na kuzifanya endelevu.
- Hutambua sehemu zilizo dhaifu na kuchukua hatua ya kuziimarisha.
- Hufahamu bidhaa zinazohitajika kwa wateja wake ili ziwepo kila wakati
- Hujua hali yake ya fedha kwa kuweka vitabu sahihi vya kumbukumbu zote

**Aina ya umiliki wa biashara**

Mjasiriamali ni lazima awe na aina ya umilikaji wa biashara ili aweze kufanikiwa.  Aina hizo ni:

***1. Umilikaji pekee***

- Biashara inamilikiwa na kuendeshwa na mtu mmoja. Mali pamoja na faida yote ni ya mmiliki huyo. Madeni na upotevu wa aina yoyote utakaotokea ni juu yake.

***2. Ubia wa kawaida***

- Mfumo unaoruhusu biashara kumilikiwa na watu angalau wawili (2).  Kwa pamoja wanashirikiana katika kupata faida na pia kwenye hasara yoyote ile itakayopatikana kutokana na mapatano ambayo watakuwa wameyaandika kwa makubaliano. Wafanyabiashara walioko kwenye ubia mna haki ya kisheria kulindana na kuangaliana kwenye utendaji. Ulipaji wa kodi kwa wenye ubia hulipwa kutokana na hisa, hii ni pamoja na faida lakini hakuna kodi ya ubia.

***3. Ushirika***

- Ushirika ni kitu chenyewe haswa chenye uhalali na haki kisheria, tofauti na wewe mwenyewe na watu wengine wanaomiliki ushirika ambao wana hisa.

**Wazo la biashara**

**Maana ya wazo la biashara**

Kabla mtu hajaanza biashara, huwa anaanza kupata wazo la nifanye nini? Mawazo haya hupitia hatua kuu mbili:

**Hatu ya kwanza**

Mawazo mbalimbali humiminika kichwani kwa mfano: *sijui jinsi ya kuanzisha duka, sijui kuuza nyama, sijui kufanya usafi.*

Mawazo ya namna hii huitwa mawazo ghafi kwani hayajachujwa. Pamoja na hayo, mawazo haya hayajafanyiwa uchunguzi wa awali kama yatatekelezeka.  Kama utaanzisha biashara katika hatua hii, uwezekano wa kuanguka ni mkubwa.

**Hatua ya pili**

Wazo ghafi hutathiminiwa, na kama litaonekana kuwa linaweza kutekelezeka kuwa biashara kamili huitwa wazo muafaka. Pamoja na kuwa na wazo muafaka, mafanikio ya biashara hutegemea uwezo wa mtekelezaji au mtafutaji.

Kubuni wazo la biashara ni muhimu kwa mtafutaji kwasababu sababu zifuatazo:

- Ni hatua ya kwanza kabla ya kuanza biashara yoyote ile.
- Ni muhimu ili kufanya biashara ifanikiwe.
- Mara kwa mara wateja hubadilika na kupendelea viu vingine ambavyo ni tofauti na vile vilivyopo.
- Mabadiliko ya tekinolojia ni endelevu.
- Athari zinazoikabili biashara yako.
- Ni muhimu kwa mafanikio ya biashara yako.
- Kutokana na mianya na nyanja za biashara pindi zinapojitokeza.

- Hali duni ya maisha.
- Ongezeko la mahitaji ya watu.

**Namna ya kupata wazo la biashara**
Mawazo mengi ya kuanzisha biashara yoyote huanzia au hutokana na mambo yafuatayo:
- Uzoefu kutoka katika familia.
- Kuhamasika kutokana na kutembelea maonyesho ya biashara wilayani, mikoani, na hata kimataifa.
- Kufanya ziara sehemu nyingine za nchi za nje na kuona watu wengine wanavyofanya.
- Kuona kwenye luninga na kusoma katika magazeti pamoja na majarida yanayoeleza mambo ya biashara.
- Kujiunga na vikundi, jumuiya na hata vilabu mbalimbali vya biashara.
- Upenzi wa vitu mbalimbali.
- Matukio kama vile gharika au majanga.
- Hali ya uchumi inaweza kumfanya mtu aingie kwenye biashara ili aweze kupata faida ya kumudu maisha.

**Utekelezaji wa wazo la biashara**
Ili wazo la biashara liweze kutekelezwa, yako mambo makuu matano ya kufanya:

**1. Mpangilio wa wazo la biashara kwa mfano**
- Aina / hali ya biashara unayoiwaza
- Nani atakayemiliki biashara hiyo – familia, ubia, kikundi n.k.
- Aina ya leseni inayohitajika – glosari, vileo, mgahawa, duka n.k.

**2. Bainisha soko kwa kutilia maanani mambo yafuatayo**
- Aina ya bidhaa/huduma utakayotoa na kwa wateja gani?
- Mbinu zitakazotumika ili uweze kuwa tofauti na washindani wako ili biashara ivutie wateja.
- Njia bora zaidi ya usambazaji na uuzaji.
- Eneo bora na nafuu kwa biashara yako.
- Namna ya kutangaza biashara yako.

**3. Fikiria namna ya kupanga na kuendesha biashara yako**
- Utahitaji vifaa vipi na wauzaji wake ni nani.
- Ni huduma gani na ukarabati gani wa vifaa unahitajika.
- Malighafi utaipata kutoka wapi.
- Namna ya kuchagua na jinsi ya kuwamotisha wafanyakazi ulionao.
- Fikiria namna ya kupanga uzalishaji na uuzaji wa bidhaa zako.

**4. Uchambuzi wa fedha**
- Chambua gharama za uzalishaji.
- Upangaji wa bei.
- Fanya makisio ya faida na hasara.
- Fanya makisio ya kitega uchumi na mtaji wa kazi.

**5. Mipango**
- Weka mipango na hatua za kuchukua ili kuanza utekelezaji kidogo kidogo.
- Pangilia fedha iliyopo.
- Panga hatua za kutekeleza wazo la biashara.
- Pangilia kwa makini huduma inayohitajika na mahali inapopatikana.
- Bainisha njia mbalimbali za kupata fedha kwa njia ya vitega uchumi.

**Jinsi ya kutambua wazo zuri la biashara**
Wazo zuri humwezesha mfanya biashara mtafutaji kufanikiwa. Hivyo basi, ni vizuri kufahamu jinsi ya kupima mafanikio. Mafanikio ya biashara hupimwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- Faida ipatikanayo
- Kutokwama kwa biashara.
- Kupanuka na kukua kwa biashara.
- Kumnufaisha mteja.

**Matatizo yanayoathiri wazo la biashara**

1. **Kutowiana na wazo la biashara ambako kunasababishwa na:**

- Kukosa imani ya kutosha kuhusiana na wazo hilo.
- Matatizo ya kupata leseni/kibali kinachohitajika.
- Hakuna ujuzi wa kutosha wa usimamizi na uongozi.
- Hakuna ujuzi wa kutosha wa kiufundi/kitaaluma.
- Hakuna uvumilifu wa kutosha kwa kusoma azma.

2. **Matatizo ya masoko au uuzaji hafifu ambao unaweza kusababishwa na:**

- Uchache wa wateja
- Wingi wa washindani
- Ufanisi na uwezo wa zaidi wa washindani
- Bei ya bidhaa / huduma ni ghali mno
- Bidhaa kukosa ubora unaotakiwa
- Ukosefu wa mwelekeo wa biashara ulio wazi
- Kutovumisha biashara vya kutosha.
- Eneo la biashara halipo wazi
- Ukosefu wa njia mbalimbali za kuuza bidhaa hiyo.

3. **Matatizo ya Uongozi**

- Uchache wa wafanyakazi wenye ujuzi na motisha ya kutosha.
- Bei za mali ghafi kuwa juu.
- Kushindwa kuzalisha bidhaa zenye ubora.
- Uzalishaji hafifu.
- Ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi.
- Kutosimamia matumizi ya fedha, malighafi na vifaa vingine.

4. **Usimamizi mbaya wa fedha**

- Wadaiwa wengi.
- Wadai wengi (kulipwa mara moja)
- Kiwango kidogo cha fedha.
- Kutotunza hesabu vizuri.

5. **Ukosefu wa mipango**

- Hakuna mipango ya muda mrefu.
- Hakuna vitega uchumi vipya.
- Kutokujua jinsi ya kupanga na kutengeneza bidhaa mpya.

**Jinsi ya Kuanzisha Biashara**

**Mchanganuo wa biashara na umuhimu wake**
Mchanganuo wa biashara ni muhimu sana kufanywa na Wajasiriamali kuwezesha biashara zao

kufanikiwa. Kuwa na mchanganuo wa biashara huwafanya kuweza kuthibitisha uhalali wa kupata mkopo pale wanapo uhitaji, kupata wawekezaji wa kushirikiana nao pia kutambua kama wanapata faida au hasara. Mchanganuo wa biashara pia humwezesha Mjasiriamali kuweka mambo yake vizuri zaidi kabla ya kuanzisha biashara.

**Utayarishaji wa mchanganuo wa biashara**
Ili kufanikisha utayarishaji wa mchanganuo wa biashara ni sharti kutoa kipaumble kwenye maeneo muhimu yafuatayo:

- Taarifa binafsi za mjasiriamali.
- Aina ya biashara itakayofanyika (huduma au bidhaa)
- Mahali itakapofanyika
- Soko linalokusudiwa
- Kuwa na taarifa kuhusu watafutaji wengine wanaotoa huduma kwenye soko linalokusudiwa.
- Mkakati utakaoiwezesha biashara hiyo ifanikiwe.
- Mahitaji ya fedha, makadirio ya mauzo na gharama za uendeshaji.
- Jumla ya wataalam watakaohitajika.
- Chanzo cha mtaji wako kuendesha biashara hiyo - Je, ni kukopa; akiba yako; ubia n.k.

**Vipengele vya mchanganuo wa biashara**
Mchanganuo wa biashara lazima utimize yafuatayo:

- Ueleze ni biashara gani unafanya
- Kwa ajili ya soko gani (wateja ni nani)
- Ni nani wanaohudumiwa kwa sasa
- Una mkakati gani wa kuwapata wateja hao
- Utekelezaji wake utakuwaje
- Je fedha zitatumikaje kukidhi mahitaji ya biashara.

**Faida ya mchanganuo wa biashara**
Mchanganuo wa biashara utakuwezesha:

- Kujua kama bidhaa au huduma yako itanunuliwa.
- Kujua watu wengine wanaofanya sawa na wewe unachotaka kufanya, wanafanyaje.
- Kujua kama kulingana na gharama zitakazoingia, bei utakayopanga itakuwa katika uwezo wa wateja wako.
- Kuona kama unapata faida au hasara.
- Kujua wapi panahitaji marekebisho.
- Kurahisisha utekelezaji
- Benki kuona umuhimu wa kukopesha.
- Kupanga vizuri mipango ya baadaye hivyo kukupa maono ya uelekeako.

**Vyanzo vya taarifa za biashara**

***1. Wateja unaowategemea***
Hawa wanaweza kutoa taarifa juu ya bidhaa na huduma ambazo wangependa kuzipata kutoka kwako. Waulize wateja wanahitaji nini na pia pata mawazo yao juu ya uzuri na pia udhaifu wanaouona kwenye biashara yako.

***2. Wasambazaji***
Hawa pia ni watu muhimu katika kutoa tarifa ya jinsi unavyofanikiwa kwenye biashara na wana uwezo wa kutoa mapendekezo ya jinsi gani unaweza kuboresha biashara kutokana na kuwa na malighafi zenye ubora na gharama ndogo.

***3. Washindani***
Shida nyingine za kibiashara zinafanana, na mara nyingi watafutaji wanakuwa tayari kuzizungumzia pamoja na wenzao haswa pale ambapo bidhaa na huduma hazishindani. Kwa kufanya hivyo watafutaji hupata faida na hatimaye kuboresha uendeshaji wa biashara zao kwa washindani, hupata taarifa za uwezo na pia udhaifu wao.

***4. Wataalam***
Hawa hutoa taarifa muhimu bila ya kuhitaji/kudai malipo kwa mfano Benki, Washauri wa Biashara, Wahasibu, Afisa Ushirika, Afisa Ushuru, Afisa Ardhi, Afisa Afya, Mwanasheria. Kazi zao zinaweza zikahitaji malipo kama leseni, viwanja lakini ushauri hutolewa bure.

**Masoko**

**Utangulizi**
Soko la mazao ya mifugo na kilimo hususani, maziwa na mazao ya maziwa, mboga na matunda hubadilika mara kwa mara kutokana na ukweli kuwa mazao yake huharibika baada ya muda mfupi, kama hayatahifadhiwa ipasavyo, pia hutegemea wingi wake, uzito wake na pia msimu wa uzalishaji.

**Mchanganuo wa soko**
Soko ni falsafa ya biashara inayosema, biashara yoyote inatakiwa kuelekeza nguvu zake katika kuwaridhisha wateja na matakwa yao. Ni kuwapatia wateja wako, vitu wanavyohitaji kwa njia ambayo itakupatia faida pamoja na kuwaridhisha wateja. Ni kuwa na vitu sahihi, kwa watu wanaohusika kwa bei sahihi, kwa wakati vinapohitajika na mahali vinapohitajika.

Baadhi ya biashara zinatokana na mwelekeo wa soko na baadhi zinatokana na mwelekeo wa uzalishaji. Zile za mwelekeo wa soko hutegemea kile kinachoweza kuuzwa na wakati zile za mwelekeo wa uzalishaji hutegemea kinachozalishwa.

Ni dhahiri kwamba biashara inayolenga kwenye matakwa ya wateja ina uwezekano mkubwa wa kukua na kuendelea kwa mafaniko makubwa.

**Kuandaa Mchanganuo wa soko**
- Kadiria ukubwa wa soko lako
- Wingi wa wateja watarajiwa, uwezekano wa kupanuka na kukua
- Malengo ya mkakati huo.
- Aina ya bidhaa (mtindo, aina, ubora)
- Bei ya kuuzia.
- Namna ya kutangaza biashara yako – kuvumisha biashara
- Bidhaa ziwafikieje wateja.
- Utaratibu wa kupata matatizo ya wateja
- Muda utakaopita kabla hujaweka mkakati mwingine.

**Soko ni muhimu kwani humuwezesha Mjasiriamali kupata taarifa zinazohusu**
- Wateja wake.
- Bidhaa iliyoko sokoni kwa wakati ule
- Mahali bidhaa inapohitajika.
- Washindani wake - hawa ni wafanyabiashara ambao wanauza bidhaa ndani ya soko hilo hilo unakouzia bidhaa zako na kuwa bidhaa hizi zinafanana na zile za kwako kwa hali moja au nyingine.

**Mambo muhimu ya kuzingatia kwenye soko**

1. **Gundua wateja wanataka nini**
- Ufanisi
- Unafuu wa bei
- Ukaribu
- Starehe
- Usalama
- Ubora wa bidhaa/huduma

2. **Wateja wako wananunua wakati gani?**
- Asubuhi, mchana au jioni
- Mwanzoni au mwishoni mwa juma
- Mwanzoni au mwishoni mwa mwaka

3. **Ni wanunuzi wa aina gani?**
- Kiasi wanachonunua kwa kipindi fulani
- Mara ngapi wanakuja
- Wanapenda kukopa au wanalipa moja kwa moja

4. **Biashara gani utauza kwa mwezi?**
- Biashara yako inashindana na nani na wako wapi hao unaoshindana nao?
- Je wanaathiri biashara yako?
- Je nini kinachokupa nafuu kwako?
- Bei zao.
- Kipimo wanachofunga (kikubwa au kidogo)
- Masharti yao.

5. **Je bei zako utapangaje?**
- Utafuata bei za serikali?
- Utaangalia bei wanazouzia wafanyabiashara wengine?
- Utakadiria bei mwenyewe kulingana na gharama?
- Utaweza kupunguza bei au itakuwa haibadiliki?
- Utaratibu gani utatumia kukopesha?
- Mtu akinunua bidhaa nyingi, je atapunguziwa bei?

6. **Kulielewa soko lako**
- Unapoingia kwenye biashara, ni vyema kutathmini soko. Hii itakusaidia kujua kama kuna soko la bidhaa unayozalisha au huduma unazotarajia kutoa.

7. **Ni nani wateja wako wa sasa na ni nani ambao ni wa uhakika kwako**
- Wateja wako ni watu wa aina gani? Kwa mfano umri wao, kipato na elimu yao, vitu wanavyopenda na mahitaji yao.
- Wanaishi wapi, na wanapendela kununua nini?

8. **Kuitangaza biashara**

Kuitangaza biashara ni muhimu ili kupata wateja. Matangazo husaidia katika kumtambulisha mfanyabiashara mwenyewe na kuifanya biashara itambuliwe na umma.

Uwezekano wa kuongeza kiwango cha mauzo pamoja na mapato upo haswa kwa kutumia matangazo kupitia vyombo vya habari, mbao za matangazo, vitini na vijitabu vyenye kurasa chache. Lengo kuu la kuvitumia vyombo vya habari ni kuongeza mauzo na mwishowe faida ya biashara.

**9. Namna ya kuuza**

Maonesho ya biashara ni moja ya chombo ambacho mfanyabiashara anaweza kutumia katika kunadi biashara yake. Kufanya hivyo kunampa mfanyabiashara fursa ya kuungana na wanamaonesho kwa nia ya kuuza bidhaa na sio kuonyesha tu. Maonesho hukupa fursa ya kujenga uhusiano na wateja wapya, kuimarisha uhusiano na wateja waliopo na pia kujitanua kwenye masoko mapya.

**10. Usambazaji bidhaa/huduma zako kwa wateja**

Mambo yafuatayo yatakusaidia kutoa uamuzi sahihi kutokana na hali halisi ya mazingira na uwezo wako kifedha:

- Je utawapelekea wateja wako walipo?
- Utatumia wachuuzi?
- Je wateja watakufuata ulipo?
- Je utatumia gharama kiasi gani?

**Mipango ya Uwekezaji**

**Mipango ya fedha na uwekezaji katika biashara**

Mipango ya fedha ni muhimu katika kupanga biashara yoyote. Ili mipango yako ya fedha ieleweke vizuri jitahidi kujibu maswali yafuatayo:

1. Mtaji kiasi gani ungehitaji kuwekeza katika biashara.

Jibu…………………………………………………………

2. Je, wewe binafsi unao mtaji kiasi gani kwa kuweka kwenye biashara tajwa.

Jibu…………………………………………………………

3. Ni vitu gani ambavyo unatarajia kununua na kuwekeza katika biashara hii.

Jibu…………………………………………………………

4. Ni gharama kiasi gani, toa x kiasi gani unazotakiwa kutoa katika maandalizi haya

Jibu…………………………………………………………

5. Je unatenga kiasi gani kwa matumizi ya dharura.

Jibu…………………………………………………………

Jumla ya gharama kwa vipengele 3+ 4+ 5 = S.

Tofauti ya kipengele 2 na S itakupa upungufu wa fedha zako ambazo unatakiwa kuwa nazo kabla ya kuanza biashara, hivyo basi itakulazimu kumtafuta mkopo.

Fedha za ziada zinazotakiwa utazipata wapi?
Je, mipango yako hii ya fedha umeifikiria kwa kutumia msaada wa mtaalam wa mambo ya fedha?

Ili kukusaidia katika kuweka mipango madhubuti ya fedha zingatia mambo yafuatayo:

- Kumbuka mara kwa mara kuongeza gharama za mambo ya dharura.
- Fikiria juu ya mtaji mkubwa wa kutosha .
- Weka makisio ya vitu ambavyo vitachangia katika uwezekaji wako.

**A. Mahitaji ya mtaji wa muda mrefu**

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Kodi ya pango, gharama za usajiri | |
| Gharama za majengo mapya/kukarabati yaliyozeeka | |
| Vifaa vya maabara/karakana | |
| Mashine za usindikaji | |
| Vifaa vinginevyo | |
| Gharama za awali za kuanzisha biashara | |
| Gharama za kutangaza biashara | |
| Malipo ya awali - kodi ya nyumba | |
| Jumla ndogo | |

**B. Mahitaji ya mtaji wa muda mfupi**

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Bili za kila mwezi (umeme, maji, simu, usafiri nk) | |
| Manunuzi ya mara kwa mara | |
| Gharama za biashara | |
| Gharama za uendeshaji | |
| Jumla ndogo | |
| Jumla ya mtaji unaohitajika A + B | |

**Mipango ya fedha**

Mipango thabiti ya fedha hukupa ufahamu wa kiasi cha fedha unachohitaji kwa kuanzia na kuendesha biashara yako. Mipango itakuwezesha kufahamu mahali ambako fedha hiyo itaweza kupatikana.

Vipo vyombo vingi vya fedha hapa nchini na nje ya nchi ambavyo kutokana navyo unaweza kupata fedha kwa ajili ya biashara yako. Usiwe mwoga wa kukopa ili mradi unalipa mikopo hiyo bila ya kuchelewa. Pia njia ya kuwa unajiwekea akiba/pesa kidogo kidogo kwenye sanduku la chuma/mbao hukusaidia kupata mtaji.

**Vyombo vya fedha vya ndani**

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Mtaji binafsi | |
| Pesa taslim | |
| Mtaji wa mali (ardhi, majengo n.k) | |
| Michango ya wanachama | |
| Mtaji wa ujenzi | |
| Jumla ndogo | |

**Vyombo vya fedha vya nje**

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Mikopo ya muda mrefu | |
| Mikopo ya benki | |
| Mikopo ya bima | |
| Mikopo toka kwa ndugu | |
| Mikopo toka kwa mashirika yasiyo ya serikali | |
| Mikopo ya muda mfupi | |
| Mikopo ya hawala za benki | |
| Jumla ndogo | |

**Mipango ya faida**

Sababu mojawapo ya kazi za kujitegemea ni kufanikisha maendeleo yako mwenyewe. Lengo ni kupata kipato kitakacho kufanya uendelee kuishi na wakati huo huo biashara iendelee kuimarika na kukua. Biashara isiyokuwa na faida ni sawa na mchezo wa kujiburudisha tu. Hivyo, ni dhahiri kuwa faida hazishuki kama mvua, faida hupangwa.

"Utabiri wa mauzo" mauzo hayana budi kuifidia gharama na matumizi yote ya biashara na hapo hapo kuachia faida.

**Kwa mfano, utabiri wa mauzo ya miezi sita ijayo:**

| Mwezi | Januari | Februari | Machi | Aprili | Mei | Juni | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo yanayotarajiwa | | | | | | | |
| Bei ya kila bidhaa (Tsh) | | | | | | | |
| Lengo la mauzo | | | | | | | |

**Utabiri wa mauzo**

Yapo mambo mawsili ya kuzingatia kwenye utabiri:

- Wingi wa bidhaa/ huduma zitakazotolewa.
- Bei utakayo toza kwa kila bidhaa / huduma.

**Kuna mambo makuu matatu ya kutilia maanani wakati wa kupanga bei**

Gharama za kuianzisha na kuendeleza biashara yako. Bei unazotoza hazina budi kuweza kuzifidia gharama zote ulizozitoa katika kuianza na kufanikisha biashara hiyo.

Bei wanazotoza washindani wako. Unaweza kuziwekea bidhaa zako bei ya chini au ya juu kulingana na ama uzuri wa bidhaa hiyo, aina ya wateja uliyo nao au aina ya washindani ulionao. Uwezo wa kununua walionao wateja wako.

**Kuchambua faida**

Chambua faida kwa kuanzia kwenye mauzo

| Shughuli | | Thamani (Tsh) |
|---|---|---|
| Thamani ya mauzo | | |
| | | |
| | | |
| Jumla ya mauzo | A | |

### Gharama za uendeshaji biashara

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Gharama za vifaa | |
| Gharama za vibarua, umeme, maji n.k | |
| Gharama za ununuzi na usambazaji | |
| Gharama za utawala | |
| Mishahara ya wanaushirika | |
| Michango mingine | |
| | |
| Jumla ndogo B | |

### Gharama za mahali pa kufanyia biashara

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Kodi ya nyumba au eneo | |
| Maji | |
| Umeme | |
| Kuyahudumia mazingira | |
| Jumla ndogo C | |

### Vyombo vya usafiri

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Leseni ya barabara | |
| Bima | |
| Ripea na matengenezo madogo madogo | |
| Gharama za uendeshaji | |
| Makato ya halmashauri ya mji | |
| Jumla ndogo D | |

### Gharama za kifedha

| Shughuli | Thamani (Tsh) |
|---|---|
| Riba ya mkopo | |
| Makato ya huduma za benki | |
| Kodi | |
| Jumla ndogo E | |
| Jumla ya gharama zote - B + C + D + E = F | |
| Faida ya biashara | |

| | |
|---|---|
| Faida ya biashara = A - F | |

TOA ZAWADI PIA

HEIFER INTERNATIONAL

TANZANIA

*Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi:*

Heifer International Tanzania
Plot 129 Block 21
Col. Middleton Road, Kaloleni,
S.L.P. 1648,
Arusha

Simu: +255 27 250 6805
Nukushi: +255 27 254 4686
Baruapepe: hpitz@heifertz.org